epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Alhamisi Mei 2, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581664
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22

**'MICHEZO MITATU ITATUPA UBINGWA'**

MEI MOSI

# Nuru mpya kikokotoo, nyongeza ya mshahara



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango

• **Mpango** asema serikali imesikia, SMZ yaahidi kutatua kero za wafanyakazi kwa wakati... *Endelea ukurasa 2&4*



Wafanyakazi wa Taasisi ya UTT AMIS, wakiandamana na bango lenye ujumbe mbalimbali, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

UKURASA WA 4

**WANANCHI WATOLEWA HOFU UCHAGUZI SERIKALI MITAA**

UKURASA WA 5

**BEI YA MAFUTA PETROLI YAPAA, DIZELI YASHUKA**



MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)...

UKURASA WA 19

**MUSEVENI AMPIGIA DEBE MTOTO WAKE, ASEMA ANA NIA YA KUBORESHA JESHI**





## Wanaojifungua watoto njiti kuongezewa likizo

UKURASA 2

## Afya ya akili tishio vijana, watoto Zanzibar

UKURASA 17

**MICHEZO** SIMBA YAWEKA REKODI MATOKEO MABAYA UK.24

**KATUNI** UK.6




Vijana wa Arusha maarufu kama 'wadudu', wakipita na mabango mbele ya Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani yaliyofanyika kitaifa, jijini Arusha jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Nuru mpya kikokotoo, nyongeza mshahara

**Na Waandishi Wetu,** ARUSHA

NI ahadi ya matumaini baada ya Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango kuzungumzia hoja ya kikokotoo cha mafao ya wastaafu kuwa imepokewa na kuahidi itafanyiwa uchambuzi zaidi.

Aidha, nyongeza ya mshahara, Dk. Mpango aliwataka wafanyakazi kuendelea kutega sikio kwa sababu Rais Samia Suluhu Hassan atasema jambo hivi karibuni.

Alitoa kauli hiyo jana wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) yaliyofanyika kitaifa katika Jiji la Arusha, akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema serikali imepokea hoja kuhusu kubadilisha kanuni ya kikokotoo kwa wastaafu kwa ajili ya kuifanyia uchambuzi zaidi kwa kuwa wafanyakazi hawaridhishwi na kanuni hizo.

"Rais Samia Suluhu Hassan, Mama wa Taifa; ameaniagiza niwaambie wafanyakazi wa Tanzania kuwa endapo hali hii itadumu, wafanyakazi wawe na matumaini kwamba atasema jambo hivi karibuni," alisema.

Kuhusu kodi ya kima cha chini cha mshahara kwa sekta binafsi, Dk. Mpango alisema, tayari serikali imeanza utafiti ambao utajumuisha sekta ndogo.

Kutokana na uhitaji huo, Dk. Mpango alitoa wito kwa wajumbe wa bodi kutoka Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Nchini (TUCTA), kushiriki kikamilifu mchakato huo ili kufikia uamuzi shirikishi utakaosadifu mazingira ya wakati uliopo.

**WATUMISHI H/SHAURI**

Dk. Mpango alisema kuanzia Julai mwaka huu, watumishi 473 kutoka Halmashauri 101 ambazo zilibainika kutokuwa na uwezo wa kulipa mishahara watumishi wake kwa kutumia mapato ya ndani sasa watalipwa kupitia mfuko mkuu wa hazina.

**SSRA KUREJESHWA**

Vilevile, Dk. Mpango, alisema serikali imesikia hoja ya kutaka kurejeshwa Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA), ikiwa ni miaka mitano tangu ilipovunjwa na majukumu yake kutwaliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

**BIMA YA AFYA**

Dk. Mpango alisema serikali imefanya maboresho katika orodha ya taifa ya dawa muhimu pamoja na miongozo mbalimbali ya tiba, hivyo kutokana na maboresho hayo, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), umefanya maboresho katika kitita chake ili kwenda sambamba na miongozo hiyo kwa lengo la kuboresha huduma bora kwa wanachama wake.

Kwa mujibu wa Dk. Mpango, kutokana na changamoto zilizojitokeza baada ya kuanza utekelezaji wa kitita hicho, serikali iliunda kamati huru ya wataalamu ili kupitia hoja za wadau na kupata suluhu ya changamoto zilizojitokeza.

**KIKOKOTOO**

Dk. Mpango alisema: "Serikali imepokea ushauri uliotolewa. Hata hivyo ni muhimu kuzingatia kwamba uendeshaji na usimamizi wa mifuko ya hifadhi ya jamii ni suala la sayansi ya watakwimu bima."

Hata hivyo, alisema serikali inawategemea wataalamu washauri kuhusu suala hilo la uhimilivu na uendelevu wa mifuko ya hifadhi ya jamii.

Alisema serikali iliposhauriwa na wataalamu iliamua kulipa deni la mifuko ya hifadhi ya jamii Sh. trilioni 2.147 hatua ambayo imeimarisha mifuko hiyo.

**KODI YA MSHAHARA**

Kuhusu mapato yasiyo ya mshahara, Dk. Mpango alisema: "Naomba nieleze kwamba kodi katika mapato ya wafanyakazi inatozwa kwa mujibu wa sheria na utaratibu wa ukokotoaji na ukusanyaji unazingatia kanuni za msingi za utozaji kodi ikiwamo kuweka usawa kwa watu wenye kipato kinachofanana."

Alisema uratibu huo unawezesha baadhi ya vitendo vya waajiri wasio waaminifu kufanya udanganyifu wa kupunguza kiasi cha msingi cha mshahara na kuainisha kwenye mahesabu yao kiasi kikubwa cha posho na marupurupu ili kukwepa wajibu wa kulipa kodi na masuala ya pensheni za wafanyakazi wao.

**NYONGEZA MSHAHARA**

Dk. Mapango alisema serikali itaendelea kuhuisha viwango vya mishahara kwa kuzingatia uwezo wa kiuchumi na kibajeti pamoja na ujazi na utendaji wa waajiriwa. Misingi hii ni muhimu ili kuepuka kuchochea mfumuko wa bei, kuhatarisha uhimilivu wa deni la taifa na athari nyingine kwenye utulivu wa deni la taifa kwa ujumla.

Naye Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Nchini (TUCTA), Tumaini Nyamhokya, aliitaka serikali kurudisha kitita cha zamani cha matibabu kinacholalamikiwa na Watanzania, ili kumaliza malalamiko kwa wanachama ambao wengi wao ni watumishi wa umma.

Alisema suala la kikokotoo, TUCTA inakiri kushiriki katika mabadiliko kilichokuwa cha asilimia 50 na 25, ambacho walijadili, mara ya kwanza kilienda kwenye asilimia 25 kwa wote. Katibu Mkuu wa TUCTA, Henry Mkunda, alisema pamoja na maboresho ya viwango vya mishahara kufanyika baada ya kusimama kwa miaka sita, bado hawikidhi kukabiliana na hali ngumu ya maisha.

Aidha, alisema gharama za maisha zimepanda kunakosababishwa na kupanda kwa bidhaa na vitu vingine muhimu hususani vyakula, matibabu, usafiri, mafuta na vifaa vya ujenzi.

***Imeandikwa na Godfrey Mushi na Cynthia Mwilolezi**


## REGIZ COMPANY LIMITED

Court Brokers, Debt Collectors, Auctioneers, Commission Agents & General Trading.

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**REGIZ COMPANY LIMITED** KWA IDHINI TULIYOPEWA NA **TPC LIMITED SUKARI ROAD S.L.P 93 MOSHI.** TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA MAGARI/MALI KAMA INAVYOONYESHA HAPO CHINI KWENYE JEDWALI. MNADA UTAFANYIKA KATIKA KIWANDA CHA TPC MOSHI SIKU NA TAREHE TAJWA.

| NO. | MALI ZITAKAZOUZWA KATIKA MNADA | TAREHE/MUDA |
|---|---|---|
| 1 | FORD DOUBLE CAB (1), FORD PICK-UP SINGLE CAB (6), MITSUBISHI CANTER (1), NISSAN UD (1), VOLVO (1), RENAULT LORRY (1), CRAWLER CAT (1), BELL FRONT END LOADER (1), KOMATSU FRONT END (1), FRONT END LOADER SKID STEER (1), HEAVY TRACTORS, CASEFERTILIZER APPLICATOR REAPER (1), SLASHER (2), AIR COMPRESSOR (2), BRUSH CUTTER (3), CHAINSAWA (3) NA GENERATOR (4). PIA KUTAKUWA NA VIFAA VINGINEVYO KAMA SPEA NA FURNITURES N. K | 15/05/2024 SAA 03:00 ASUBUHI - 10:00 JIONI |

**MASHARTI YA MNADA:**

1. Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% ya bei siku ya mnada na kiasi cha pesa kilichobaki kilipwe ndani ya masaa 48. Kinyume na hapo kiasi kilichotolewa hakitarudishwa na Mnada utarudiwa.
2. Magari/ Mali yatauzwa kama ilivyo na mahali yalipo.
3. Gharama za kubadilisha Hati Miliki (Transfer of Ownership) na gharama nyingine ikiwemo usafiri zitakuwa ni za Mnunuzi.
4. Mali yoyote itakayouzwa chini ya milioni moja ni lazima malipo yake yafanyike kwa asilimia 100% na mali iondolewe siku iyoiyo.
5. Kukagua mali Tarehe 06 na 07 Mwezi Mei 2024 kuanzia saa nne asubuhi mpaka saa kumi jioni.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI; PIGA SIMU-0789 900 006**
**EMAIL; info@regiz.co.tz/ Website; www.regiz.co.tz**

**WOTE MNAKARIBISHWA**


# Wanaojifungua watoto njiti sasa kuongezewa likizo

**Na Romana Mallya**

KILIO cha wafanyakazi wanaojifungua watoto njiti kuongezewa muda wa siku za likizo ya uzazi, kimepatiwa ufumbuzi baada ya serikali kutangaza likizo hiyo kuanza mtoto atakapomaliza kipindi cha uangalizi maalum daktari atakapothibitisha afya yake imeimarika.

Serikali imefafanua kuwa iwapo mfanyakazi atajifungua mtoto au watoto njiti, kipindi cha uangalizi maalum hakitahesabiwa kama likizo ya uzazi.

Mwezi Machi mwaka huu, Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE) kiliomba serikali kufanya mabadiliko katika sheria zake ili kuwaongezea muda wa siku za likizo ya uzazi wafanyakazi wanaojifungua watoto njiti.

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akizungumza jana katika Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi (Mei Mosi) yaliyofanyika jijini Arusha, alisema likizo ya uzazi ni miongoni mwa haki za mfanyakazi ambazo hutolewa kwa siku 84 endapo mfanyakazi atajifungua mtoto mmoja au siku 100 endapo atajifungua zaidi ya mmoja.

"Iwapo mfanyakazi atajifungua mtoto au watoto kabla ya muda wake (njiti). Mtoto au watoto husika huwekwa kwenye chumba na mashine maalum chini ya uangalizi wa madaktari na wahudumu wengine wa afya hadi pale wataalam hao watakapojiridhisha afya ya mtoto au watoto hao imeimarika," alifafanua.

Dk. Mpango alisema iwapo mfanyakazi atajifungua mtoto au watoto njiti kupindi cha uangalizi maalum hakitahesabiwa kama likizo ya uzazi. Alisema likizo ya uzazi itaanza pale mtoto atakapomaliza kipindi cha uangalizi maalum daktari atakapothibitisha.

Vilevile, alisema mfanyakazi husika, ataruhusiwa kutoka kazini saa saba na nusu kila siku kwa muda wa miezi sita, baada ya kumalizika kwa likizo ya uzazi ili kumpa fursa ya kwenda kunyonyesha.

Alisema kwa upande wa likizo ya uzazi kwa wafanyakazi wa sekta binafsi, serikali inatambua umuhimu wa kulinda haki ya mama na mtoto na hususan watoto njiti.

"Serikali ipo katika hatua ya kuifanyia marekebisho Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini Sura 366, ili likizo ya uzazi ianze pale mtoto atakapomaliza kipindi cha uangalizi maalum daktari atakapothibitisha.

Ofisa Elimu Kazi wa TUGHE, Nsubisi Mwasandende, kupitia taarifa yake kwa vyombo vya habari mwezi Machi, alisema lengo ni mfanyakazi kupata fursa ya kuwahudumia watoto hao, sambamba na kupata muda wa kupumzika ili wanaporejea kazini waweze kulete tija katika maeneo yao ya kazi.

## KUMBUKUMBU

# TUNAMSHUKURU MUNGU KWA MAISHA YAKE



# DR. REGINALD MENGI

29 MEI, 1942 - 2 MEI, 2019

## PUMZIKA KWA AMANI

IPP
Cares For You



Mwakilishi wa Jumuiya ya Kimataifa ya wanawake wanaoishi na virusi vya UKIMWI (VVU) Afrika Mashariki (ICWEA), Dk. Tatu Nyange (katikati), akizungumza katika semina ya kuwajengea uwezo wanafunzi machampioni sita wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, ili kuwa mabalozi kwa wanafunzi wengine kujilinda na UKIMWI, iliyoratibiwa na Taasisi ya Dignity and Wellbeng for women Living With HIV in Tanzania (DWWT), chuoni hapo Kigamboni, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SMZ yaahidi kutatua kero za wafanyakazi kwa wakati

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema itaendelea kutatua kwa wakati changamoto zote za wafanyakazi kwa wakati, ikiwamo kutoa posho ya nauli ya Sh. 50,000 kwa wafanyakazi watakaostahili, kutoa huduma bora kwa wananchi na kuendelea kukuza uchumi wa nchi

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyasema hayo jana kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) yaliyofanyika Uwanja wa Gombani, Chakechake, mkoa wa Kusini Pemba.

Pamoja na ahadi hiyo, Rais Dk. Mwinyi aliiagiza Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, kukutana mara nne kwa mwaka na vyama vya wafanyakazi wakiwamo wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Zanzibar (ZATUC) ili kutatua kwa haraka changamoto za wafanyakazi badala ya kusubiria kila mwaka wakati wa maadhimisho.

Dk. Mwinyi alisema serikali pia itaendelea kuwahimiza wafanyakazi kuheshimu na kutekeleza kwa vitendo misingi ya haki za binadamu na utawala bora.

Alisema iwapo wafanyakazi watazingatia misingi hiyo kwenye utekelezaji wa majukumu yao, ufanisi wa kazi utaongezeka. Pia alisema serikali itazidi kuhakikisha mazingira ya kazi na maslahi ya wafanyakazi yanaimarika ili kuongeza ufanisi kazini.

Alisema ndani ya kipindi cha miaka mitano, serikali imejipangia kutengeneza ajira 300,000 kwa wananchi wake kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 - 2025.

Ndani ya kipindi cha miaka mitatu, alisema serikali kupitia shughuli mbalimbali za utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa barabara, shule, vituo vya afya na hospitali, bandari, miundombinu ya maji na umeme , ajira mpya 187,651 sawa na asilimia 104 ya lengo la ajira 180,000 zimepatikana.

Kuhusu kuimarisha mazingira bora ya wafanyakazi Zanzibar, Rais Dk. Mwinyi alisema, Serikali inaendelea kuimarisha maslahi ya wafanyakazi ikiwemo mishahara, upandishwaji madaraja, nyongeza za mwaka, posho, fidia, nauli kwa wenye kustahiki pamoja na matibabu.

"Napenda niwahakikishie kuwa serikali ina dhamira ya dhati ya kuendelea kuimarisha mazingira ya kazi na utoaji wa maslahi bora kwa wafanyakazi." Alisema Rais Mwinyi.

Katika utekelezaji wa dhamira hiyo, alisema serikali itachukuwa hatua, kuanza kutoa posho la nauli za kwenda kazini na kurudi nyumbani ya Sh. 50,000 kwa watumishi wote wanaostahili kulipwa na kwamba Sh. 34,099,500,000 zimetengwa na Serikali kwa ajili ya posho la usafiri.

Aidha, Serikali imedhamiria kuhakikisha inaongeza fedha kwa ajili ya posho ya likizo na jumla ya Sh. 2,523,814,700 zimetengwa na Serikali kwa ajili ya likizo katika bajeti mpya ya mwaka wa fedha 2024/25.

Alisema, serikali ni sikivu na inaendelea kutoa maslahi na kuimarisha mazingira ya kazi kwa lengo la kuleta ufanisi na maendeleo ya nchi yetu. Pia alisema serikali haitosita kuzitatua changamoto za wafanyakazi na watu wote kwa kadri ya uwezo wake ili kulinda hadhi na heshima yao.

Lengo ni kupata maslahi bora ya Utumishi na jamii kwa ujumla kwa kutoa huduma stahiki na kuinua uchumi wa nchi.

Kuhusu madeni ya nauli kwa wanaofanya kazi maeneo ya mbali hususani walimu, Rais Dk. Mwinyi alifafanua baada ya kuondoshwa kwa ugatuzi wa mwaka 2021 alisema tayari ulipwaji wa nauli hizo umeanza kutolewa kwa walimu wa Skuli za Msingi baadae hatua zitaendelea na kwa walimu wa shule za serikali.

Akizungumzia suala la wafanyakazi kukatwa kodi nyingi kwenye mishahara yao, kiinua mgongo na pensheni Rais Dk. Mwinyi alisema serikali kupitia Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji imefanya ufuatiliaji wa hoja hiyo na kubaini kuwa ipo kwa mujibu wa sheria na kanuni za fedha zilizopo.

Hoja ya kuwepo kwa wafanyakazi wa mkataba wa muda mfupi katika Mabaraza ya Manispaa, Miji na Halmashauri. Tayari suala hili limejadiliwa kupitia vikao vya pamoja na taasisi husika ili kulipatia ufumbuzi, alisema serikali imezitaka taasisi zinazohusika kurekebisha kasoro zilizopo kwa kufuata kwa sheria za kazi.

Pia alihimiza suala la kudumisha amani, utulivu, maelewano na mshikamano katika sehemu za kazi. Pia alihimiza wafanyakazi wote kutokufanyakazi kwa mazoea na kuwasihi wajiepushe na rushwa na ubadhirifu ili uchumi ukue zaidi.

Kuhusu kuimarisha upatikanaji wa ajira za nje ya nchi, Rais Mwinyi alisema serikali zimejitahidi sana kwenye eneo hilo na serikali ya Tanzania imetia saini mkataba wa ushirikiano na Qatar na Saudia na sasa iko katika hatua za mwisho za kutia saini mkataba na Oman.

Akizungimzia upatikanaji wa ajira hizo, alisema umeongezeka kwa asilimia 35 kutoka ajira 1,080 kwa mwaka 2022/2023 hadi ajira 3,078 kwa mwaka 2023/24 na ajira za ndani zimeongezeka kwa asilimia 65.9 kupitia mikataba iliyothibitishwa kutoka ajira 6,348 mwaka 2022/23 hadi 9,630 kwa mwaka 2023/24.

Pia alisema kwa serikali kuu, ajira 6,735 zimetolewa kwa watumishi kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita.

Kuhusu uwekezaji, Dk. Mwinyi alisema ni miongoni mwa vyanzo vya upatikanaji wa ajira za ndani ya nchi na imeimarika.

Akizungumzia miradi mipya iliyotoa ajira, Dk. Mwinyi alisema kwa mwaka wa fedha wa 2023/24, miradi 63 imesajiliwa yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 1,499 na inatarajia kutoa ajira zipatazo 4,392.

Aidha, alisema serikali ilitoa Sh. bilioni 15 kwa ajili ya programu ya Inuka yenye lengo la kutoa mikopo kwa wajasiriamali na kwa sasa programu hiyo tayari imetoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 22.4 kutokana na fedha za marejesho ambazo zinaendelea kutolewa mikopo mipya na kuzalisha ajira za moja kwa moja kwa wananchi 43,360.

Kuhusu programu ya Mfuko wa Khalifa (Khalifa Fund) alisema nayo imetoa mikopo ya Sh. bilioni 2.10 kwa miradi 18 na kuwanufaisha wananchi 19,373 waliojiajiri

Pia alisema Mfuko wa Bima ya Afya Zanzibar (ZSHF), alisema serikali imeimarisha afya za wafanyakazi na familia zao kwa kuimarisha sheria ya mfuko huo na wategemezi wao wapatao 187,641 walikuwa wamesajiliwa kwenye mfuko huo na kufanya idadi ya wanachama 236,570 hadi sasa.

Akizungumzia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) alisema serikali imetekeleza ahadi kuanzisha mafao mawili mapya kwa wafanyakazi wake likiwamo fao la kuumia kazini na fao la upotevu ajira kwa wanachama wake wakiwamo wafanyakazi wa sekta zote pamoja na mafao mengine.

Pia alisema serikali imeanza kuwalipa wastaafu wote kima cha chini cha pensheni kuanzia 180,000.

Kadhalika, kwa kuzingatia wafanyakazi wanaostaafu kwa hiari wakiwa na umri wa miaka 55 watapata kiinua mgongo kamili badala ya pungufu kama ilivyokua awali.

## Wananchi waondolewa hofu uchaguzi wa Serikali za Mitaa

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni, amewahakikishia Watanzania kuwa uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika mwaka huu pamoja na Uchaguzi Mkuu mwakani, utakuwa huru bila kuwapo vihatarishi vya uvunjifu wa amani.

Masauni amesema kila mtu atapata haki yake ya kidemokrasia ya kuchagua na kuchaguliwa bila kuwapo kwa vihatarishi vya amani katika maeneo yote uchaguzi utakapofanyika.

Alitoa kauli hiyo jana baada ya kufungua Kikao cha Baraza Kuu la Wafanyakazi wa wizara hiyo kilichofanyika Makao Makuu ya Jeshi la Magereza, Msalato jijini, Dodoma. "Niwahakikishie wananchi, tumejipanga vizuri kuelekea uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu mwakani. Niwaombe Watanzania watege masikio kuelekea bajeti ya wizara ambayo tutaiwasilisha bungeni katikati ya mwezi unaokuja.

"Tunaenda kuboresha takribani kila sehemu katika vyombo vyetu vya usalama hasa Jeshi la Polisi, tunaenda kuliboresha katika kila sehemu ikiwamo vifaa na mambo mengine mbalimbali," alisema. Waziri Masauni aliwataka wananchi kutokuwa na wasiwasi kuhusu uchaguzi ujao kwa kuwa Jeshi la Polisi liko vizuri kuhakikisha demokrasia inaendelea kutekelezwa katika misingi ya amani na utulivu na watu wanachagua na kuchaguliwa bila bughudha yoyote, huku nchi ikiendelea kubaki salama.

Akizungumzia chaguzi hizo, Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini, IGP Camillus Wambura, alimpongeza Waziri Masauni kwa kusimamia ongezeko la bajeti kwa wizara na vyombo vyake.

Alisema ongezeko hilo linakwenda kuboresha utendaji kazi hasa wa Jeshi la Polisi kuelekea pia uchaguzi wa Serikali za Mita na Uchaguzi Mkuu.

"Mwaka huu tunakwenda kuingia kwenye uchaguzi na mwaka kesho uchaguzi mkuu, wizara yetu ina nafasi kubwa sana kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru na wa haki, kwa hiyo niwaombe wajumbe kutambua kwamba, hii ngoma bado ni ya kwetu na mpiga ngoma ni Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo tukae tayari kucheza ngoma hiyo ili kuhakikisha chaguzi zote mbili zinapita salama," alisema.

Mkutano huo wa Baraza la Wafanyakazi uliongozwa na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Ally Gugu, mambo mbalimbali kuelekea bajeti ya wizara yalijadiliwa huku akiwataka watumishi kuwa wabunifu, waadilifu na kutekeleza maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya utolewaji wa huduma sahihi na zisizo na upendeleo kwa wananchi.

## HABARI KITAIFA

# Bei ya petroli juu, dizeli chini

**Na Jenifer Gilla**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imetangaza bei mpya za mafuta zilizoanza kutumika jana huku bei ya rejareja ya petroli ikiongezeka kwa Sh. 57 kulinganisha na mwezi uliopita na dizeli ikishuka kwa Sh. 14.

Taarifa ya mamlaka hiyo ilieleza kuwa mabadiliko ya bei za mafuta kwa Mei ,2024 yamechangiwa na ongezeko la bei za petroli iliyosafishwa katika soko la dunia (FOB) kwa wastani wa asilimia 3.90 na kupungua kwa wastani wa asilimia 1.31 kwa mafuta ya dizeli.

Imetaja sababu nyingine kuwa ni kupungua kwa gharama za uagizaji mafuta kwa wastani wa asilimia 7.21 kwa petroli na asilimia 2.15 kwa dizeli kwa Bandari ya Dar es Salaam, asilimia 10.14 kwa petroli na asilimia 23.18 kwa dizeli kwa Bandari ya Tanga na wastani wa asilimia 5.32 kwa mafuta ya petroli na dizeli kwa Bandari ya Mtwara.

"Aidha, mabadiliko hayo yamechangiwa na kubadilika kwa kiwango cha kubadilishia fedha za kigeni na kuendelea kutumia 'EURO' kulipia mafuta yaliyoagizwa," ilieleza sehemu ya taarifa ya EWURA.

Taarifa hiyo imeonyesha kuwa bei ya jumla ya mafuta yanayochukuliwa katika Bandari ya Dar es Salaam, petroli imepanda hadi kufikia Sh. 3,181.48 kwa lita kutoka Sh. 3,125.27 iliyotangazwa mwezi uliopita, huku dizeli ikishuka hadi Sh. 3,063.68 kutoka Sh. 3,077.94.

Kwa mkoa wa Tanga, bei ya jumla ya petroli sasa itauzwa Sh. 3,184.05 kutoka Sh. 3,129.50 na dizeli Sh. 3,069.46 kutoka Sh. 3,085.59. Mkoa wa Mtwara petroli itauzwa Sh. 3,185.05 kutoka Sh. 3,128.03 na dizeli Sh. 3,067.90 kutoka Sh. 3,079.23.

Kutokana na hali hiyo, bei ya rejareja ya petroli kwa Dar es Salaam imepanda kwa Sh. 57 huku dizeli ikishuka kwa Sh.14, hivyo petroli kwa rejareja kwa mkoa huo sasa itauzwa Sh. 3,314 kutoka Sh. 3,257, huku dizeli ikiuzwa Sh. 3,196 kutoka Sh. 3,210 .

Katika mkoa wa Tanga, bei ya rejareja ya petroli sasa ni Sh. 3,360 kutoka Sh. 3,303 huku dizeli ikiuzwa Sh. 3,242 kutoka Sh. 3,256. Mtwara, petroli ni Sh. 3,317 kutoka Sh. 3,260 na dizeli inauzwa Sh. 3,200 kutoka Sh. 3,212.

Taarifa hiyo imeonyesha bei ya bidhaa hizo rejareja kwa sasa kwa mikoa mingine ikiwamo Arusha ambayo petroli ni Sh. 3,398 huku dizeli ikiuzwa Sh. 3,280, Mara Petroli ni Sh. 3,479 na Dizeli Sh. 3,362, na Sumbawanga mkoani Rukwa Petroli ikiuzwa Sh. 3,487 na dizeli Sh. 3,369.




Mkurugenzi wa Furniture Centre, Prasad Kumar (kushoto), akikabidhi cheti cha utendaji bora upande wa masoko kwa Ofisa Mkuu wa Masoko wa kampuni hiyo, Ganesh Raghunathan (kulia), wakati wakiadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wadau wa viwanda watoa mbinu kukuza pato la taifa

**Na Maulid Mmbaga**

WADAU wa viwanda wametoa rai kwa serikali kuweka kipaumbele katika kuwezesha upatikanaji wa vifaa mbalimbali vinavyotumiwa wakati wa kutengeneza bidhaa viwandani ili fedha zinazotumika kwenye ununuzi nje zibaki nchini kwa lengo la kuchagiza ukuaji wa pato la taifa.

Rai hiyo ilitolewa jana Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya utengenezaji wa samani za ndani ya Furniture Centre, Prasad Kumar, wakati wa hafla ya kusherehekea siku ya wafanyakazi duniani.

Alisema katika kutekeleza majukumu yao, wamekuwa wakipata shida kuagiza vifaa mbalimbali nje ya nchi kwa zaidi ya miaka 10.

Kumar alisema kuna vitu vingi wanavihitaji zikiwamo 'screw', bawaba na gundi, ambavyo alisema wanaagiza kutoka mataifa mengine kwa sababu hakuna kiwanda chochote kinachotengeneza nchini.

Alisema endapo mamlaka zitaliangalia hilo na kulifanyia kazi, haitawasaidia wao tu bali itakuwa chachu ya kuongezeka kwa mapato serikalini.

"Katika utengenezaji wa samani za ndani, vitu vingi vinahitajika lakini kinachopatikana Tanzania ni mbao pekee. Vingine tunanunua kwenye mataifa mengine, hivyo nishauri serikali iangalie ni vitu gani havipatikani ili ihamasishe watu kuwekeza katika utengenezaji wa vifaa hivyo ili vipatikane hapa nchini.

"Hiyo itasaidia kukuza sekta ya viwanda nchini, wawekezaji, na kampuni nyingi zinazokuja Tanzania lazima zitahitaji samani za ndani na ofisini, hivyo serikali iendelee kuweka mazingira rahisi ya upatikanaji vifaa hivyo, ili iwe rahisi kuzalisha bidhaa zaidi," alisema Kumar.

Akizungumzia kuhusu wafanyakazi, Meneja wa Masoko wa kampuni hiyo, Ganesh Raghunathan, alisema wameandaa hafla hiyo lengo likiwa ni kuonyesha kuthamini watumishi wao ambao wanashirikiana katika kukuza kampuuni yao sambamba na uchumi wa taifa.

"Bila wao hatuwezi kufikia malengo tulijojiwekea na hata katika uchumi wa taifa, wafanyakazi ni watu wanaopaswa kupewa kipaumbele cha kwanza kwani wanafanya kazi kila siku, hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi. Kwetu sisi bila hawa hatuna mafanikio.

"Tunafanya kazi kama familia na tunazingatia kanuni zote ikiwamo mazingira salama ya kazi. Tunawashukuru sana kwa sababu bila wao hatungeweza kuwa hapa tulipo. Tunawapatia zawadi kila mwezi kama njia ya kuendelea kuwaongezea motisha ya utendaji wao kazini," alisema Raghunathan.

Mmoja wa wafanyakazi wa kampuni hiyo, Wahida Hassan, alitoa wito kwa waajiri kuwaangalia zaidi katika kuwaongezea mishahara kutokana na kuongezeka kwa gharama za maisha pamoja na kuwapatia bima ya afya ambayo itawasaidia katika kupata huduma za matibabu.

International School of Tanganyika
Challenge | Support | Inspire

Elementary Campus
elementary@istafrica.com
+255 684 228 882/3
United Nations Road

Secondary Campus
secondary@istafrica.com
+255 787 997 778/98
Haile Selassie Road
Dar-es-salaam, Tanzania

## INVITATION FOR BIDS

Bids are invited from interested registered, competent, reliable and licensed suppliers/dealers to provide the under listed goods and services for the year ending 31st July 2025.

| S/N | Category No. | Description |
|---|---|---|
| 1. | Category 01 | Maintenance Materials |
| 2. | Category 02 | Consumables and Cleaning Materials |
| 3. | Category 03 | Stationeries |
| 4. | Category 04 | Staff Welfare Supplies (Sugar, Tea, Coffee & Milk Powder) |
| 5. | Category 05 | Timber |
| 6. | Category 06 | Electrical Appliances (Fridges, Cookers & Air-conditions) |
| 7. | Category 07 | Motor Vehicle spare parts, Oil & Filters |

**Conditions:**

- Bid document(s) will be emailed to the bidders on payment of TZS. 50,000/= payable per bid category. Payments should be made to the Billing Department located in the Administration Building (Gate #5), off United Nations Road, Upanga, between 10.00 am to 1.00 pm Monday to Friday. Bidders will need to provide the School with the email ID at the time of making payment. Once payment has been received, bid documents will be emailed by the following working day.
- Bids should be emailed to **bids@istafrica.co.tz** latest by 2 p.m. on **Friday, May 17th, 2024.** No bids will be accepted after this time. In addition, bidders should attach scanned copies of certificates of registration, business license, TIN/VAT certificates and User Identification Number certificate (for VAT registered suppliers). On submission of the information, the bidders would receive a confirmation that IST has successfully received their bids.
- The School is not bound to accept the lowest or any bid and reserves the right to reject all or any of the bids received.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Neema kwa kinamama wanaojifungua watoto njiti

**KATIKA** maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani iliyoadhimishwa jana, serikali imetangaza kuwa kinamama wanaojifungua watoto njiti likizo yao inaanzia pale watoto watakapokuwa wametimiza miezi tisa ya kuzaliwa.

Hapo mwanzo mama akienda kujifungua ilikuwa haijalishi kama mtoto huyo amezaliwa kwa wakati au kabla na likizo yake ya kujifungua ilikuwa ikihesabika miezi mitatu kama Sheria ya Kazi inavyosema.

Kwa kuzingatia kauli hiyo ni kuwa kinamama waliokuwa wakijifungua watoto njiti walikuwa wakipunjika muda wao wa likizo kwa kuwa mtoto ambaye alikuwa amezaliwa kabla ya wakati kwa mfano amezaliwa miezi miwili kabla, mama huyo ilimbidi arudi kazini baada ya miezi mitatu wakati mtoto huyo ndio alitakiwa kupokewa duniani.

Kinamama wengi walikuwa wakipitia wakati mgumu, kwa kuwa ilikuwa ikiwalazimu kutoka kazini mapema ili kwenda kuwahudumia watoto wao.

Kila mtu anafahamu malezi ya watoto njiti yalivyo magumu kutokana na kuhitaji uangalizi wa hali ya juu na wengine mama hulazimika kumlea kwa kuwa naye kifuani muda wote ili kupata joto la mama badala ya kuwekwa kwenye mashine ya kuwasaidia kupata joto.

Wanawake wengine iliwalazimu kuacha kazi kwa sababu ya kukosa wasaidizi nyumbani wa kumsaidia kumwangalia na kumpa matunzo mazuri mtoto huyo.

Kwa hili la likizo ya kinamama wanaojifungua njiti kuongezwa limeleta tumaini kubwa kwa wanawake wengi.

Baadhi walikuwa wanaona kama kujifungua mtoto njiti ndio mwisho wao wa kufanya kazi kutokana na jukumu la kumlea mtoto huyo.

Wengi walikuwa wanakosa haki zao za msingi za kufanyakazi kwa ajili ya kupata kipato cha kutunza familia kwa kusaidiana na mwenza wake.

Kwa wale ambao walijifungua watoto hao wakiwa hawana ndoa, walipitia wakati mgumu zaidi kutokana na wenzao kuwakimbia kwa kuogopa matunzo na kuwaachia mzigo kinamama.

Mwezi Machi mwaka huu, Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE), kiliomba serikali kufanya mabadiliko katika sheria zake, ili kuwaongezea muda wa siku za likizo ya uzazi wafanyakazi wanaojifungua watoto njiti.

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akizungumza jana katika Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi (Mei Mosi) yaliyofanyika jijini Arusha, alisema likizo ya uzazi ni miongoni mwa haki za mfanyakazi ambazo hutolewa kwa siku 84 endapo mfanyakazi atajifungua mtoto mmoja au siku 100 endapo atajifungua zaidi ya mmoja.


"Iwapo mfanyakazi atajifungua mtoto au watoto kabla ya muda wake (njiti). Mtoto au watoto husika huwekwa kwenye chumba na mashine maalum chini ya uangalizi wa madaktari na wahudumu wengine wa afya hadi pale wataalam hao watakapojiridhisha afya ya mtoto au watoto hao imeimarika," alifafanua.

Dk. Mpango alisema iwapo mfanyakazi atajifungua mtoto au watoto njiti kupindi cha uangalizi maalum hakitahesabiwa kama likizo ya uzazi.

Hizi ni habari njema kwa kinamama na kwakweli watoto wanahitaji malezi makubwa kutoka kwa wazazi wao kwani muda huo ndio humuunganisha mama na mtoto zaidi na kutengeneza upendo.

Hivi kipindi hicho ni muhimu kwa kinamama wote na wanastahili kupata likizo hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Ajenda za kutokomeza malaria zianzie vikao vyetu tunakoamua



Na Yasmine Protace

**UGONJWA** wa malaria asili yake hadi sasa, ni tatizo linalochangiwa na mdudu mbu wa aina ya anopheles. Mazingira rafiki yanayopaswa kutumika, ni kuepuka unyevu katika mazingira yanayokuzunguka.

Kuendekeza hayo, kunachangia kufuga mazingira rafiki yanayozalisha mbu waenezao malaria. Ndio maana kuna jitihada zinafanywa na serikali, hata ngazi kimataifa, kupambana na malaria.

Jitihada hizo ni pamoja na kuhakikisha elimu ya usafi wa mazingira, inatolewa kuhakikisha jamii inakuwapo katika mazingira safi na salama, katika maeneo husika. Kumekuwapo shughuli za usafi kwa kila kata nchini kila wiki, wenyeji wakitakiwa kufanya usafi wa mazingira, ili kuhakikisha maeneo yao yanakuwa salama.

Naibu Waziri wa Afya Dk. Godwin Mollel, hivi karibuni, ameziasa Kamati za Ulinzi na Usalama nchini kuona umuhimu wa kuifanya ajenda ya kutokomeza malaria, iwe ya kudumu kwenye vikao vya maamuzi.

Dk. Mollel alitamka hayo, akimwakilisha Waziri wa Afya Ummy Mwalimu kwenye kilele cha Siku ya Malaria Duniani, iliyofanyika mkoani Tabora, akisema nchi imeendelea kupiga hatua katika vita hivyo, ikilinganishwa na miaka zaidi ya 20 iliyopita, maambukizi na vifo vya malaria, vilikuwa kati ya asilimia 45 hadi 50.

Ni hapo Naibu Waziri huyo, aliyezama katika fani hiyo ya tiba, akafafanua kuwa azma ya serikali ni kufikia asilimia 3.5 ifikapo mwaka ujao 2025 na maambukizi kutoweka kabisa mwaka 2030.

> **Ni hapo Naibu Waziri huyo, aliyezama katika fani hiyo ya tiba, akafafanua kuwa azma ya serikali ni kufikia asilimia 3.5 ifikapo mwaka ujao 2025 na maambukizi kutoweka kabisa mwaka 2030.**

Nakumbuka akadokeza; "Leo tunazungumza asilimia 8.1 kama nchi, lakini miaka ya 1998, tulikuwa na kiwango cha juu sana. Hivyo, ili tuweze kufikia adhma yakumaliza kabisa malaria ifikapo 2030 kila mmoja wetu anawajibu wakufanya."

Hilo linakuwa sehemu ya msisitizo, kwamba malengo tajwa yatafikiwa pale juhudi za makusudi zitafanywa kwa ushirikiano baina ya serikali na wadau wanaohusika.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Afya Ofisi ya Rais TAMISEMI Samsoni Maella, ana maelezo kwamba Utumiaji wa Mifumo iitwayo 'GoTHOMIS' na 'FFARS' imekuwa chachu ya kukusanya takwimu sahihi kwa ajili ya ngazi ya kuamua, hali iliyochangia kufanyika uamuzi sahihi unaotoa takwimu sahihi.

"Kama Ofisi ya Rais TAMISEMI, tumefanikiwa kuimarisha miundombinu ya Afya na Rasilimali watu mathalani miaka mitatu nyuma tulikuwa na Hospitali za Wilaya 77 leo hii tunazo 177 hizi zimechochea sana uimarishaji wa huduma" anasema Mahela.

Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI Dk. Hamis Kigwangala, akatoa wito kwa serikali na wadau kuongeza afua za kutibu watoto shuleni, pia wafike maeneo ya migodi, mashamba makubwa na waliko wafugaji.

Awali, Msimamizi wa Miradi kutoka Wizara ya Afya Dk. Catherine Joachim, aliyemwakilisha Katibu Mkuu wake, anasema kuchaguliwa kwa mkoa wa Tabora kuwa Mwenyeji wa Maadhimisho ya Wiki ya Malaria, ni pamoja na kuongeza nguvu ya afua za kupambana nayo.

Anafafanua, mkoa huo una maambukizi ya juu ya ugonjwa, asilimia 23.4 sasa, kutoka asilimia 11.7 mwaka 2011.

# Taarifa mikopo 'kausha damu' kutua bungeni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI inatarajiwa kuwasilisha bungeni taarifa ya kushamiri mikopo ya 'kausha damu' kesho, baada ya wabunge kuibua hoja ya kushamiri hadi mitandaoni ikizihusisha baadhi ya kampuni za simu.

Akizungumza bungeni juzi, Spika wa Bunge, Dk.Tulia Ackson, alisema serikali inatarajia kuwasilisha taarifa hiyo Alhamisi.

Aprili 24, mwaka huu, wabunge waliibua suala hilo na kuhoji mikakati ya serikali wa kuzibana taasisi za fedha zinazotoa mikopo kwa riba kubwa, hali inayosababisha magonjwa ya afya ya akili na uvunjifu wa ndoa.

Akiuliza swali la nyongeza bungeni jana, Mbunge wa Viti Maalum, Felista Njau, alihoji mkakati wa serikali wa kukomesha mikopo ya kausha damu ili kunusuru wananchi ambao wamekuwa wakipata matatizo ya afya ya akili na ndoa nyingi kuvunjika.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alitaka kujua kuna mkakati gani ya kufuatilia na kuchukua hatua kwa taasisi za fedha zinazotoa mikopo yenye riba kubwa kinyume na muongozo wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Kadhalika, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Shally Raymond, alisema pamoja na Sheria ya BoT ya mwaka 2018 na Kanuni za Mwaka 2019, takribani mikoa 17, ukiwamo Kilimanjaro hasa wilaya ya Moshi, imekuwa ikitolewa mikopo kausha damu na kutaka kauli ya serikali.

"Kampuni za simu zimekuwa zikitoa mikopo haraka bila kujaza fomu na vijana na wanawake wajasirimali wa Kilimanjaro wamekuwa wakichangamkia fursa hiyo, Je? lini serikali italazimisha kampuni hizo kutoa elimu?" alihoji.

Kutokana na kauli hizo, Spika Tulia alisema hana uhakika kama kampuni za simu ambazo zimesajiliwa zinatoa mikopo kausha damu kama taasisi nyingine ambazo hazijasajiliwa.

"Naibu Waziri wa Fedha nakupa muda baada ya kipindi cha maswali katafute habari za uhakika hapo nje kwa kampuni za simu kama zinatoa mikopo kausha damu,"alisema.

Awali akijibu maswali ya wabunge hayo, Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande, alizielekeza taasisi zinazotoa mikopo hiyo kuacha mara moja na serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu suala hilo.

Pia aliagiza BoT kuzifuatilia taasisi zinazoenda kinyume na sheria hiyo, serikali haitakuwa na muhari kwa taasisi zinazokiuka sheria na kanuni hizo.

Kadhalika alisisitiza serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kisera, kiutawala na kisheria ili kudhibiti tabia ya baadhi ya taasisi za fedha kutoa mikopo kinyume na miongozo iliyopo.

Alisema wataendelea kutoa elimu kwa umma juu ya masuala ya fedha ili kumsaidia mwananchi kufanya maamuzi sahihi kuhusu fursa za mikopo zilizopo, viwango vya riba na athari zake, vigezo vya kuzingatia na umuhimu wa kurejesha mikopo.



Naibu Meneja wa Mradi wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Msalato mkoani Dodoma kutoka Kampuni ya Beijing Construction Engineering Group, David Dong (kushoto), akitoa maelezo kwa wahariri wa vyombo vya habari, kuhusu maendeleo ya ujenzi wa uwanja huo, walipotembelea jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Majaliwa ashuhudia utiaji saini miradi ya umwagiliaji ya bil. 258/-

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali inaendelea kuchukua hatua za kuimarisha kilimo cha umwagiliaji kwa kujenga miundombinu na kuongeza bajeti.

Aidha, amezielekeza halmashauri zote nchini kuweka mpango wa ardhi kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji.

Majaliwa aliyasema hayo jijini hapa juzi wakati wa hafla ya kutia saini mikataba ya ujenzi na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa miradi ya umwagiliaji.

Alisema bajeti katika sekta ya umwagiliaji imeongezeka kwa asilimia 677 hadi kufikia Sh. bilioni 361.5 mwaka 2023/2024 kutoka Sh. bilioni 46.5 iliyotengwa kwa mwaka 2021/2022.

"Nitumie fursa hii kumpongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kutenga fedha nyingi kwa ajili ya uendelezaji wa miradi ya umwagiliaji nchini," alisema.

Aliwasisitiza watendaji wote wanaohusika na utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji wafanye kazi kwa ufanisi na wazingatie suala la uwazi pamoja na usimamizi mzuri wa fedha.

Alisisitiza kuwa fedha hizo ni kodi za wananchi wa Tanzania zitumike kuwanufaisha Watanzania wote.

"Wakandarasi na wasimamizi wa miradi inayotekelezwa kwa force account, wahakikishe wanatoa kipaumbele cha ajira kwa wananchi walioko katika maeneo ambayo miradi hiyo inatekelezwa na wahakikishe miradi inakamilika kwa wakati kwa mujibu wa makubaliano."

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe alisema mikakati ya serikali ni kuanza kutumia maji ya Ziwa Tanganyika katika miradi ya kilimo cha umwagiliaji na hatua ya kwanza itaanza katika mikoa ya Katavi na Rukwa.

Alisema baada ya Bunge la Bajeti kutafanyika upembuzi wa kina na yakinifu ili maji hayo yasafirishwe hadi Simiyu na Tabora kwenye ukame.

"Baada ya Bunge la Bajeti kukamilika tunatarajia kuanza kuyatumia maji ya Ziwa Tanganyika katika shughuli za kilimo na uzuri mitambo tunayo naamini jambo hili litafanikiwa," alisema.

Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC), Raymond Mndolwa, alisema hafla hiyo ni kwa ajili ya utiaji saini mikataba 24 ambayo kati yake 14 ya ujenzi kwa kutumia wakandarasi yenye thamani ya Sh. bilioni 248.7, sita ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa kutumia washauri elekezi yenye thamani ya Sh. bilioni 9.35.

Alitaja miradi mingine minne itatekelezwa kwa kutumia wataalam wa ndani kutoka Tume ya Taifa ya Umwagiliaji yenye thamani ya Sh. bilioni 16.95 ambayo itatekelezwa kwa utaratibu wa Force Account.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema serikali imetoa fedha zaidi ya Sh. bilioni 67 kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa ya umwagiliaji ambayo yatahudumia ekari zaidi ya 35,000.

"Mabwawa haya ni muhimu kwa Mkoa wa Dodoma kwasababu asilimia 72 ya wananchi wanaishi kwa kutegemea kilimo hivyo yataenda kufanya mapinduzi makubwa katika sekta ya kilimo na kuinua Pato la Taifa na mwananchi mmoja," alisema.

## KABWELA — Na Fadhili Mohammed



# Aliyepinga kifungo miaka 30 kwa kubaka, afungwa maisha

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Masijala ya Moshi imemuhukumu kifungo cha maisha jela, Elineema Mwandry, aliyekata rufani akipinga adhabu ya miaka 30 jela aliyopewa na Mahakama ya Wilaya ya Siha kwa kumbaka binti yake akiwa na miaka saba.

Mwandry aliongezewa kifungo na mahakama hiyo juzi mbele ya Jaji Lilian Mongela baada ya kutupilia mbali rufani ya kupinga hukumu ya mahakama ya chini.

Ilidaiwa Mei 14, 2022 kijiji cha Lomakaa wilayani Siha, Mkoa wa Kilimanjaro, mrufani alidaiwa kumbaka binti yake mwenye umri wa miaka saba ambaye anasoma darasa la kwanza katika Shule ya Msingi Lomakaa.

Mrufani aliposomewa mashtaka alikana kutenda tukio hilo, upande wa Jamhuri ulikuwa na mashahidi watano na upande wa utetezi mrufani alikuwa na shahidi mmoja.

Ilidaiwa mara nyingi mrufani alikuwa anatumia chumba cha kulala wageni kumwingilia binti yake.

Mei 16, 2022 binti alitoa taarifa ya tukio hilo kwa rafiki yake ambaye ni shahidi wa pili na yeye alimshauri akatoe taarifa kwa dada mkuu wa shule hiyo.

Shahidi huyo pia alimshauri akatoe taarifa kwa mwalimu wa darasa ambaye ni shahidi wa tatu alifanya hivyo na shahidi huyo wa tatu pia alitoa taarifa kwa Mwalimu Mkuu wa shule hiyo ambaye ni shahidi wa nne.

Baada ya taarifa hizo kufika kwa uongozi wa shule walitoa taarifa Polisi na Mei 23, 2022 mrufani alikamatwa na kushtakiwa kwa kubaka.

Shahidi wa tano ambaye ni daktari alimfanyia uchunguzi binti na kubainisha katika ripoti yake kwamba aliingiliwa na kitu kutokana na sehemu ya siri kuongezeka ukubwa.

Katika utetezi wake mrufani alidai hakuwa akiishi na mama wa binti huyo ambaye alimwambia atakuja kumfanyia kitu kibaya ambacho hatakisahau.

Alidai kesi hiyo imetengenezwa hakuwahi kufanya tukio hilo.

Akipinga adhabu ya miaka 30 jela aliyopewa na Mahakama ya Wilaya ya Siha baada ya kumtia hatiani alitoa sababu nne.

Alidai Mahakama ilikosea kumuhukumu na kumtia hatiani wakati hakukuwa na uthibitisho wa umri halisi wa mtoto, ilikosea pia kuegemea katika ushahidi wa shahidi wa kwanza na wapili.

Alidai Mahakama ilikosea kumtia hatiani kwa mashtaka ambayo hayakuthibitishwa bila kuacha shaka na upande wa Jamhuri na kwamba Mahakama hiyo haikuzingatia utetezi wake wakati inatoa hukumu.

Mahakama baada ya kusikiliza hoja hizo na majibu ya Wakili wa Serikali Henry Daudi, ilitoa uamuzi.

"Kuhusiana na ushahidi wa shahidi wa pili unaodaiwa kukinzana na ushahidi wa shahidi wa kwanza, ningependa kusema kwamba sio mikanganyiko yote inaweza kuathiri ushahidi katika kesi.

"Katika suala lililopo mbele yetu, shahidi wa pili taarifa yake ilikuwa kuhusiana na kile shahidi wa kwanza alikuwa amemwambia.

"Kwa wazi huo ulikuwa uvumi, hakuwahi kuwapo kwenye tukio lolote ambapo shahidi wa kwanza aliingiliwa na mrufani.

"Kwa kweli, sioni madai ya kupingana na chochote kilichosemwa na mwathiriwa kuhusu ubakaji, matukio yaliyofanywa kwake na mrufani.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nicolaus Mkapa (wa pili kulia), akikabidhi tuzo ya ushindi wa kwanza katika sekta ya madini kwa mtaalamu wa masuala ya usalama wa Barrick, Aristides Medard, katika hafla ya kukabidhi tuzo jijini Arusha juzi. Wengine ni wafanyakazi wa Barrick. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kortini madai ya kusafirisha dawa za kulevya

**Na Grace Gurisha**

MKAZI wa Mbezi jijini Dar es Salaam, Nasibu Kisebengo (44), amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa tuhuma za kusafirisha heroin na cocine kinyume cha sheria.

Akisoma hati ya mashtaka juzi, Wakili wa Serikali, Happy Mwakanyamale, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Ushindi Swalloh, alidai kuwa mshtakiwa huyo anatuhumiwa kwa mashtaka matatu ya kusafirisha dawa za kulevya ndani ya Jiji la Dar es Salaam.

Mwakanyamale alidai kuwa katika shtaka la kwanza, Kisebengo anatuhumiwa Februari 27, 2024 alikutwa eneo la Feri Tatavamba ndani ya Wilaya ya Kigamboni, Dar es Salaam akisafirisha dawa za kulevya aina ya heroin gramu 5.76.

Alidai kuwa, katika shtaka la pili mshtakiwa alikutwa eneo hilo na tarehe hiyo akituhumiwa kusafirisha dawa za kulevya aina ya cocine gramu 0.82.

Aliendelea kudai kuwa, Februari 28, 2024 mshtakiwa akiwa eneo la Mbezi Zone Makaranga, Wilaya ya Ubungo, Dar es Salaam alikutwa akisafirisha dawa za kulevya aina ya heroin gramu 20.96.

Mshtakiwa alikana kuhusika na tuhuma hizo, Wakili Mwakanyamale alidai kuwa hakuna dhamana kutokana na mashtaka anayotuhumiwa nayo.

Pia alidai kuwa upelelezi bado unaendelea na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa kwa kesi hiyo na kuangalia hatua ya upelelezi ilipofikia. Hakimu Swalo ameahirisha kesi hiyo hadi Mei 14, 2024 kwa kutajwa.

# LSF, Stanbic zatia saini kuleta ushirikiano miradi maendeleo

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI isiyo ya kiserikali ya The Legal Services Facility (LSF) kwa kushirikiana na Benki ya Stanbic Tanzania, zimetia saini makubaliano ya ushirikiano wa kutekeleza miradi ya maendeleo yenye lengo la kuwainua wanawake na wasichana kiuchumi, kielimu na kiafya.

Mkataba huo wa miaka miwili unalenga kuweka juhudi na rasilimali za pamoja kati ya taasisi hizo ili kukabiliana na changamoto za kijamii, hasa zinazowakabili wanawake na wasichana.

Makubaliano hayo yanalenga zaidi katika kuweka mazingira mazuri ya elimu na kuboresha afya ya uzazi pamoja na kuwawezesha wanawake kupata fursa za kiuchumi, elimu ya kifedha, pamoja na kuwaunganisha kwenye fursa za kupata mitaji kwa ajili ya kuwawezesha kiuchumi.

Lengo kuu la mashirikiano hayo ni kuhakikisha fursa sawa, kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake ili waweze kutimiza ndoto zao.

Maeneo haya yanawiana kati ya vipaumbele vya benki hususan katika miradi yake ya kijamii pamoja na dhamira ya LSF ya kukuza haki ya kijamii kwa maendeleo endelevu. Aidha, ushirikiano huo utachangia moja kwa moja katika kufanikisha kipaumbele cha Taifa na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs); 5 (Usawa wa Jinsia), 3 (Afya Bora na Ustawi), 4 (Elimu ya Ubora), na 16 (Amani, Haki na Taasisi Imara).

Mkurugenzi Mtendaji wa LSF, Lulu Ng'wanakilala alisema; "Tunajivunia kusaini mkataba huu leo ambao unatilia mkazo dhamira yetu ya kuwakutanisha wadau husani mashirika binafsi ili kuunga mkono juhudi za pamoja katika kutatua changamoto za jamii kwa njia inayoleta tija na matokeo endelevu. Makubaliano haya tunaoingia leo yatarahisisha utekelezaji wa miradi ya pamoja na kukuza fikra shirikishi katika kuweka miradi na mipango mipya pamoja na kuendeleza yale ambayo yalishawekwa kabla.

Kwa hivyo, nachukua fursa hii kuishukuru Benki ya Stanbic kwa kushirikiana nasi. Napenda hasa kuwashukuru kwa mradi wa elimu na afya ya uzazi, ambao utatekelezwa kupitia mbio za kila mwaka za Run for Binti. Tunayofuraha kuwa na mshirika muhimu katika mbio za mwaka huu. Kupitia ushirikiano huu, tunaamini kabisa kuwa tunaweza kufikia walengwa zaidi kuliko hapo awali."

Mtendaji Mkuu wa Benki ya Stanbic, Manzi Rwegasira alisema; "Tuna furaha kubwa kushirikiana na LSF ili kufanikisha miradi itakayowezesha vijana na wanawake katika jamii kote nchini, pamoja na kukabiliana na athari za mazingira kwa kupanda miti ili kuchangia malengo ya nchi yetu yaTanzania katika kulinda mazingira. Ushirikiano huu unalenga kuimarisha fursa za kiuchumi kwa wanawake na vijana kupitia mipango inayozingatia ujuzi wa kifedha na maendeleo ya biashara. Ili kuwezesha kuimarisha ujuzi kwa walengwa, tunalenga kutoa rasilimali zinazohitajika katika kuleta uhuru na mafanikio endelevu ya kifedha.

"Tuna furaha kufanya kazi pamoja na LSF haswa katika kuendeleza mipango hii, ambayo inachangia moja kwa moja katika mipango ya maendeleo endelevu ya nchi yetu. Tunatazamia kuleta matokeo chanya na endelevu kwenye maisha ya wanawake, vijana, na jamii zote za Tanzania."



# Tanzania yatetea tuzo utalii Afrika

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

MAMLAKA ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) imezindua kampeni ya siku 131 ya upigaji kura kuwania tuzo ya kivutio bora cha utalii Barani Afrika kwa mwaka 2024 inayoandaliwa na Mtandao wa World Travel Awards (WTA).

Mwaka jana, NCAA ilishinda tuzo hiyo ya WTA baada ya kuibuka kinara katika kinyang'anyiro hicho kilichohusisha vivutio vingine vya Table Mountain, Harbeestpoort Aerial Cable Way, V & A Waterfront na Ruben Island ya Afrika Kusini.

Vivutio vingine vilivyoshindanishwa mwaka 2023 na NCAA, ni Ziwa Malawi, Okavango Delta ya Botswana, Pyramids of Giza ya Misri pamoja na Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (KINAPA).

Akizindua kampeni hiyo jijini Arusha jana, Kaimu Kamishna wa Uhifadhi wa NCAA, Victoria Shayo, alisema zoezi hilo lilianza mwishoni mwa mwezi uliopita na linatarajiwa kukamilika Septemba mwaka huu. "Hii tuzo ina umuhimu mkubwa katika kuendeleza sekta ya utalii nchini na duniani. Nitoe rai kwa Watanzania na wageni wote wanaoitembelea Tanzania kuipiga kura nyingi kwa Ngorongoro ili kuiwezesha Ngorongoro kutetea taji lake," alisema. Kwa mwaka huu, nchi tano za Afrika za Tanzania, Afrika Kusini, Botswana, Misri na Malawi zinawania tuzo hiyo.

Kuhusu ongezeko la watalii nchini, Kaimu Kamishna Shayo, alisema hadi kufikia nusu ya mwaka wa fedha wa 2023/24, NCAA imepokea zaidi ya 700,000 na kuiwezesha mamlaka hiyo kupata zaidi ya Sh. bilioni 170.

Meneja wa Huduma za Utalii wa NCAA, Mariam Kobelo ameviomba vyombo vya habari nchini kuendelea kuwahamasisha wananchi kutembelea vivutio vya utalii na kupata elimu ya jinsi vilivyo.




Mbunge wa Viti Maalum wa mkoa wa Manyara, Regina Ndege (kulia), akizungumza katika semina ya matumizi ya matokeo ya sensa ya watu na makazi kwa viongozi wa serikali, wa mila na kisiasa, makundi maalum ya walemavu, wafugaji, bodaboda na wajasiliamali, mjini Babati, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Makinda ahofia wavamizi ardhi KICoB

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

BARAZA la Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) limetakiwa kuchukua hatua ya kuilinda ardhi ya Taasisi ya Elimu ya Ushirika na Biashara Kizumbi (KICoB) iliyoko Shinyanga dhidi ya uvamizi unaoweza kufanywa na wenyeji na kudhibiti mgogoro wa ardhi.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa MoCU, Anne Makinda wakati akizungumza na jumuiya ya wanazuoni wa chuo hicho wakati uzinduzi wa baraza la tatu la chuo linaloundwa na wajumbe 17.

Makinda ambaye alikuwa spika wa zamani za Bunge aliiomba MoCU kukichukulia chuo hicho cha mkoani Shinyanga kama mto kwa kufikiri nini cha kufanya.

Alisisitiza kuwa dhamana ya MoCU pia ni kujenga uchumi wa watu wadogo wadogo na si wa mashirika makubwa.

Akizungumzia kuhusu baraza hilo, alisema anatarajia litasimamia uhuishaji wa mitaala na uanzishaji wa mitaala mipya ya mafunzo itakayoendana na mahitaji ya sasa na Sera ya Elimu ya Mwaka 2014, Toleo la Mwaka 2023.

Alisema sera hiyo inatoa msisitizo kwenye ujuzi ili wahitimu waweze kuajirika, kujiajiri na kuajiri wengine.

Makamu Mkuu wa MoCU, Profesa Alfred Sife, alimweleza Makinda kuwa chuo hicho kama taasisi ina vyombo vya kufanya maamuzi ngazi mbalimbali.

Profesa Sife alisisitiza kuwa chombo kikuu ni Baraza la Chuo ambalo hufanya kazi kwa kusaidiwa na kamati mbalimbali.

Alisema baraza hilo limeundwa kwa mujibu wa Ibara ya 18 (1) ya Hati Idhini ya Chuo ya Mwaka 2015 na ukomo wa muda wa mwenyekiti ni miaka minne na wajumbe mitatu kwa mujibu wa kanuni ya 1 na 2 ya sehemu ya pili ya hati idhini ya chuo hicho.

Kabla ya uzinduzi huo, Katibu Mkuu wa zamani Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ambaye kwa sasa ni Mwenyekiti wa baraza hilo, George Yambesi, alisema idadi ya wanafunzi wanaohitimu chuoni hapo kila mwaka imefikia 3,500.

# Yatima, wazee wapewa misaada

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SHIRIKISHO la Vyama vya Wafanyakazi Nchini (TUCTA), limewaongoza watumishi wa Serikali kuwafariji yatima na wazee wasiojiweza mkoani hapa baada ya kuvipatia vituo vitatu Sh. milioni 12 kama asante ya Sikukuu ya Wafanyakazi Duniani.

Akizungumza jana wakati akikabidhi fedha taslimu na vitu mbalimbali, Mwenyekiti wa Kamati ya Michezo ya Mei Mosi Taifa, Roselyne Massam, alivitaja vituo hivyo kuwa ni cha Wazee Meru Elderly Initives kilikabidhiwa Sh.500,000, cha mabinti Kindness Children Care Sh.800,000, The Joy of God Orphanage Centre Sh.600,000 na Ummu Aisha Orphanage Centre Sh.500,000.

Alisema fedha hizo zimechangiwa na watumishi hao ambao ni wanamichezo kutoka taasisi 56 ambazo zimeshiriki michezo Mei Mosi mwaka huu.

Katibu wa michezo hiyo, Itika Mwakenja, alisema pia wamenunua umeme wa Sh.150,000 kwa ajili ya matumizi ya vituo vyao.

Alisema kwa upande wa vyakula wamekabidhi mchele, sukari,unga wa ngano, maharage, sabuni, mafuta, chumvi, taulo za kike, Pampers, madaftari, kalamu, juisi na miswaki.

Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Arusha, Denis Mgiye, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa huo, Paul Makonda, alishukuru kwa misaada hiyo kuwa itavisaidia vituo hivyo kwa kuwa imegusa mahitaji muhimu kwa mwanadamu.

Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Arumweu, Ruth Kaaya, alisema wanahudumia wazee 300 kwa wilaya nzima, kati yao 255 wamefadhiliwa na saba.

"Mahitaji yao muhimu yote wamepata leo tunashukuru sana watumishi waliojitoa kusadia wahitaji. Wazee wanaonyanyasika au kukosa mahali pa kwenda kupata msaada wanakaribishwa kupewa ushauri na njia itakayowasaidia zaidi," alisema

# TBS yawanoa wajasiriamali ubora uzalishaji bidhaa

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WAJASIRIAMALI mkoani Arusha wamesema watatumia elimu waliyopewa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) katika maonyesho ya Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) kuleta matokeo chanya ndani ya jamii.

Waliyasema hayo juzi wakati wa maonyesho hayo yaliyoanza Aprili 23 hadi 30 jijini Arusha.

Wakizungumza na waandishi wa habari baadhi ya wajasiriamali walisema wamepatiwa elimu kuhusu taratibu za kufuata ili kudhibitisha ubora wa bidhaa wanazozalisha ili ziweze kupata nembo ya ubora ya TBS.

Asha Abdallah, alisema amepata mwamko zaidi wa kuthibitisha ubora wa bidhaa anazozalisha, kwamba ameambiwa kuwa huduma hiyo inatolewa bure kwa wajasiriamali kwa gharama za Serikali.

Aidha, baadhi ya wananchi walisema kupitia elimu waliyoipata wataongeza umakini wa kuangalia muda wa mwisho wa matumizi kwa bidhaa wanayotaka kununua, kwani hivi sasa wanafahamu kwamba bidhaa zilizoisha muda wa matumizi ni hatari kwa afya.

"Uwepo wa TBS kwenye maonesho haya imekuwa ni fursa muhimu kwetu, watu wengi wananunua bidhaa bila kuangalia muda wa mwisho wa matumizi ulioandikwa kwenye vifungashio, lakini kuanzia sasa nitakuwa balozi mzuri," alisema Paul Edward.

Ofisa Udhibiti Ubora wa TBS, Mariam Maarufu alisema kupitia maonesho hayo imekuwa fursa muhimu kwa shirika kukutana na wadau mbalimbali na kuwaelezea majukumu yanayotekelezwa na TBS.

Mbali na kuwaeleza majukumu hayo, lakini pia walitoa elimu kwa wajasiriamali hao jinsi ya kuzalisha bidhaa bora ili waweze kupata alama ya ubora, ambayo itawafungulia wigo wa masoko ya ndani na nje ya nchi.

Alisema alama ya ubora ya TBS itawasaidia wajasiriamali na wazalishaji kwa ujumla kuaminika sokoni na kukubalika, hivyo kuingia kwenye soko kifua mbele, kwani bidhaa zao haziwezi kutiliwa shaka.

Aidha, aliwataka waingizaji wa vipodozi nchini, kuingiza vipodozi ambavyo vimesajiliwa na TBS ambapo kwa kutembelea tovuti ya shirika hilo, wataweza kupata orodha ya vipodozi ambavyo haviruhusiwi kuingia nchini na vile vinavyoruhusiwa.

Alisema hatua hiyo itawezesha kuwaepusha kupata hasara, kwani wanapoingiza vipodozi vilivyopigwa marufuku watachukuliwa hatua ikiwemo bidhaa hizo kuzirudisha walikozitoa au kuteketezwa kwa gharama zao.





# Watu watatu wafariki dunia kwa kuangukiwa na ukuta

**Na Halima Ikunji,** TABORA

WATU watatu wamefariki dunia kwa kuangukiwa na ukuta wa nyumba katika Kijiji cha Iyombo Nyasa Kata ya Utwigu wilayani Nzega.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Richard Abwao amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema watu hao walifikwa na umauti nyakati za usiku wakiwa wamelala, aliwataja waliofariki ni Rashidi Matoma, Chiku Mihayo na Hamisi Rashidi.

Abwao alisema tukio hilo lilitokea wakiwa wamelala na chanzo cha ajali hiyo ni mvua kubwa kunyesha na kusababisha ukuta kuwaangukia.

Alisema miili ya marehemu hao imehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhia maiti na uchunguzi wa daktari ulibaini sababu ya vifo hivyo ni majeraha makubwa kichwani baada ya kudondokewa na ukuta na damu kuvuria katika ubongo. Hivyo, alitoa wito kwa wanafamilia wanapopata matatizo wahakikishe wanakwenda kwa viongozi wa dini au wakiserikali kwa ajili ya kupata ushauri na siyo kujichukulia sheria mkononi.

Aidha, aliwaasa wananchi kuchukua tahadhari katika kipindi hiki cha mvua na kuhakikisha watoto wao wanakuwa salama na wasicheze sehemu yenye mashimo ya madimbwi.

Pia alisema katika mkoa wake hali ya usalama inaendelea vizuri japokuwa matukio machache yanaendelea kujitokeza.



Meneja wa Usajili wa Kemikali na Maabara kutoka Ofisi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Mussa Kazumila, akitoa elimu kuhusu matumizi bora ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu wilayani Misungwi, mkoani Mwanza jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ‘Matumizi nishati safi yanamkinga mwanamke kupata magonjwa’

**Na Maulid Mmbaga**

IMEELEZWA kuwa matumizi ya nishati safi ya kupikia inasaidia kulinda afya ya wanawake kuepukana kupata magonjwa kama vile saratani ya mapafu na matatizo ya upumuaji.

Vilevile inawaepusha kinamama na watoto kuumia kwa kubeba kuni nzito na kuepuka kujeuriwa na wanyama wakali wakiwa wanatafuta kuni msituni.

Hayo yalielezwa na Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Oryx Gas Tanzania, Benoit Araman wakati wa hafla ya ugawaji mitungi ya gesi na majiko kwa waandishi wa habari.

Alisema kuna faida nyingi za kutumia nishati safi ikiwemo

kuongeza ufanisi katika uzalishaji na kupunguza muda wa taasisi husika kutafuta nishati nyingine kama kuni na mkaa.

Alisema kupika kwa kutumia Oryx Gas kunalinda mazingira kwa kutokomeza ukataji wa miti, kwamba misitu ni muhimu kwa kudumisha viumbe hai, kuhifadhi udongo, kusaidia mzunguko wa maji.

Araman alisema wanatoa mitungi ya gesi na majiko kwa makundi mbalimbali lengo likiwa ni kuunga mkono serikali katika kuwezesha jamii kuachana na matumizi ya kuni na mkaa.

Alisema: “Kwa kutambua umuhimu wa nishati safi tumeamua kuibeba kampeni hii kwa ukubwa wake, Rais Samia Suluhu Hassan ameeleza dhamira yake ifikapo mwaka 2032 asilimia 80 ya Watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia”.

Meneja Masoko wa Kampuni hiyo, Peter Ndomba, alisema mwaka 2021 walianza jitihada za kuhakikisha kila kijiji nchini kinakuwa na msambazaji mmoja wa gesi, kwamba kwa sasa wanaendeleza kampeni hiyo nyumba kwa nyumba.

Alisema nchini kuna nyumba milioni 14 na kati ya hizo ni miliomi mbili tu zinazotumia nishati safi ya kupikia.

# Wadaiwa kutoroka na fedha za mauzo ya maji

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI ambao walikuwa wakisimamia mauzo ya maji kwenye vituo ya kuchotea maji katika maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Shinyanga, wamedaiwa kutoroka na fedha za mauzo.

Hayo yalibainishwa juzi kwenye kikao cha Baraza la Madiwani la Manispaa ya Shinyanga, wakati wa ajenda taarifa ya mkurugenzi kutoka kwenye taasisi za serikali, wakati wa uchangiaji wa taarifa ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA).

Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, alibainisha hayo wakati akizungumza kwenye baraza hilo, alisema watu ambao waliwekwa na SHUWASA kusimamia mauzo ya maji kwenye vituo vya kuchotea maji wametoroka na fedha za mauzo.

“SHUWASA mnapotuambia kwamba maghati hayatoi maji sababu ya madeni tunashindwa kuelewa, hebu tupeni ufafanuzi mzuri kwanini maji hayatoki, sababu taarifa tulizonazo watu ambao mliwaweka wenyewe kuuza maji ndiyo wametoroka na fedha za mauzo,” alihoji Masumbuko.

Baadhi ya madiwani akiwamo Mariamu Nyangaka wa Kitangili, walihoji kwa nini baadhi ya vituo vya kuchotea maji havitoi huduma ya maji kwa wananchi na vimefungwa kabisa.

Mkurugenzi wa SHUWASA, Yusuph Katopola, akitoa majibu kwenye baraza hilo, alisema maghati ya kuchotea maji yamekuwa na matatizo ya usimamizi, kwa watu kukosa uaminifu na kutumia fedha za mauzo ya maji.

Alisema sababu kubwa ambayo imesababisha maghati mengi kusitisha utoaji wa huduma ya maji ni madeni, kutokana na wasimamizi wake kutolipa bili za maji na kwamba kwa sasa wanachokifanya ni kuangalia utaratibu wa kuweka mita za maji za malipo ya kabla.

Alitaja sababu nyingine maghati ya maji kufungwa, kwamba matumizi ya maji kwa wananchi yamekuwa madogo, sababu baadhi wameshavuta maji majumbani mwao na hivyo kusababisha mauzo ya maji kuwa chini.

Aidha, aliwaomba madiwani wenye maeneo ambayo maghati ya maji yanahitaji zaidi kwa wananchi wawasiliane na SHUWASA ili huduma ya maji irejeshwe.

Pamoja na mambo mengine kikao hicho kilipokea na kujadili taarifa mbalimbali, zikiwamo ya Kamati ya kudhibiti Ukimwi, mipango miji, mazingira, uchumi, afya, elimu, fedha na utawala.

# Mavunde apiga marufuku polisi kupelekwa migodini

**Na Neema Sawaka,** GEITA

WAZIRI wa Madini, Antony Mavunde ameziagiza Kamati ya Ulinzi na Uslama ya Wilaya na Mkoa kuacha tabia ya kuwapeleka polisi kwenye maeneo ya migodi pindi wachimbaji wadogo wanapovumbua miamba yenye dhahabu.

Alisema tabia hiyo ya kuwapeleka polisi kwa lengo la kuwazuia wachimbaji hao kufanya shughuli zao ili kuwalinda wamiliki wa leseni waliotelekeza leseni inasababisha ugomvi kati ya wananchi na serikali.

Aliyasema hayo wakati akitatua mgogoro baina ya wamiliki wa leseni kikundi cha utulivu mining group, mwekezaji wa kampuni Xintai company ltd na wachimbaji wadogo wa mgodi wa bululu uliopo wilayani Mbogwe Mkoani Geita.

“Hatuwezi kuwafanya wachimbaji wadogo wawe watumwa kwenye nchi yao kwa kutumia ofisi ya serikali kuwagombanisha wananchi na serikali yao, mwenye jukumu la kulinda leseni ni mwenye leseni,” alisema Mavunde.

Alisema ataendelea kufuta leseni, akisema Machi 22 mwaka huu alifuta leseni 2,648 na hivi karibuni alifuta leseni 227 na ataendelea kuzifuta mpaka wakae sawa kwenye sekta hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Geita Martine Shigela katika mkutano huo alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kufuta leseni hizo na kuwapa wachimbaji wadogo.

Alisema kufanya hivyo ni kurudisha mtaji ili kusaidia maisha ya wachimbaji wadogo na maendeleo yao pamoja na kuchochea ukuaji wa uchumi kwenye Mkoa wa Geita.

ama
ALHAMISI MEI 2, 2024
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12


**Magwiji dunia wakusanyika Dar kuumiza vichwa mapambano yake**



Ukurasa 13

ZIMAMOTO & MGAMBO WA UOKOAJI...

Serikali inavyojipanga zama mpya kukabili majanga kwa staili ngeni



Ukurasa 14

USALAMA MAHALI PA KAZI

**Simulizi ya utatu wa serikali, mwajiri na mwajiriwa wanavyojitwisha wajibu wao**

AFYA

## SAMIA & TAFSIRI YA UWEKEZAJI AFYA...

# Dk. Mollel: Kiwanda mionzi kinanusuru, vifaa, teknolojia, utaalamu, miundombinu

**Na Mwandishi Wetu**

CHINI ya wiki moja imepita, tangazo la Wizara ya Afya katika tovuti yake ikifafanua 'uendeshaji wa huduma za kibingwa za wiki mbili mikoani, kati ya Aprili 29 na Mei 11', ikiwa na nukuu:

"Huu ni uwekezaji mkubwa uliofanywa na Dk. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuhakikisha mwananchi anapata huduma za kibingwa katika ngazi ya mkoa."

Ni taarifa iliyofafanua azma ya Rais katika vipaumbele vyake; kuimarisha kupatikana huduma za kibobezi, kuwapo miundombinu bora na matabibu mabingwa.

Siku mbili kabla, daktari na Naibu Waziri wa Afya, Godwin Mollel, akiwa mjini Tabora anafafanua mageuzi ya kisekta aliyofanya Dk. Samia katika sekta ya afya, yanagusa uwekezaji kwenye; teknolojia, elimu na wataalamu na vifaa vya afya vinanunuliwa kwa wingi kitaifa kufika kila kona.

Ni ufafanuzi wake Jumamosi iliyopita mjini Tabora, akimwakilisha Naibu Waziri Mkuu, Dk. Dotto Biteko, kwenye Maadhimisho ya Miaka 25 ya Huduma ya Maendeleo ya Mtoto na Kijana nchini, yaliyoandaliwa na Shirika la Kimataifa la Compassion.

Dk. Mollel anafafanua kuwa, Rais Dk. Samia ameonyesha upendo kwa jamii yake, akisogeza nyumbani huduma tiba iliyofuatwa mbali, pia teknolojia na utaalamu, sasa asilimia 97 ya huduma hizo ziko jirani.



Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alipokuwa mkoani Tabora wikiendi iliyopita. **PICHA: MTANDAO**

Hapo anatumia stadi ya fani yake akifafanua mgonjwa wa kifua, miaka minne au zaidi iliyopita nchini 'alifumuliwa' kifua chote, sasa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), sasa mgonjwa huyo wa moyo anapitiwa padogo zaidi.

Naibu Waziri anafafanua: "Dk. Samia Suluhu Hassan alikuja Muhimbili, tukamwambia tuna shida maana watu wanakaa wodini na ugonjwa wa moyo unaleta gharama katika jamii kwa kukaa muda mrefu."

Dk. Mollel, anataja faida ya bajeti yao pana, fedha zaidi ya shilingi bilioni 28 zimetolewa kununua vifaa tiba, ambavyo mgonjwa akiingizwa katika mashine, hakuna haja ya kufungua kifua na baada ya muda mfupi anaruhusiwa kurudi nyumbani.

"Tunaingia kwenye mshipa mkubwa hapa mguuni tunaelekea kwenye moyo tunakupiga operesheni, baada ya siku mbili unaelekea kwako una nda nyumbani," anatamka Dk. Mollel.

Anafafanua kuwapo wagonjwa wengi waliokuwa wakipelekwa nchini India kutibiwa na fedha nyingi zilitumika, sasa hilo linafanyika nyumbani. Kuhusu wagonjwa wa selimindu nchini, Rais Samia anatamka kuletwa teknolojia mpya ya kutibu ugonjwa huo, na ya kifafa na ufafanuzi wake:

"Leo pale Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Benjamini Mkapa (Dodoma) tunachukua kitu kwenye mifupa kwa ndugu yako ambaye hana tatizo hilo, unapandikizwa unapona," anaeleza.

Dk. Mollel anataja kuwapo waliozaliwa wana 'vibiongo', pia Rais Dk. Samia akaridhia kununua mashine maalumu, ambayo imetatua changamoto hiyo.

Eneo lingine analitaja ni kiwanda kipya cha kuzalisha mionzi tiba nchini, Tanzania ikiwa katika nchi tano pekee zilizo nazo Afrika, wakati huduma hiyo ya mionzi ilitoka nje ya nchi.Vilevile, anafafanua hadi sasa, Tanzania ina uwezo wa kugundua ugonjwa wa kansa kabla ya miaka mitano, kutokana na kuwapo mashine za kisasa zilizowekezwa na Rais Dk. Samia.

Anasema teknolojia hizo sasa zimeshuka mpaka katika ngazi ya zahanati, hata kuwasaidia wahitaji wengi katika Taasisi ya Kansa ya Ocean Road

"Juzi tumeenda na Kamati ya Bunge (ya afya), asilimia 70 wamepatikana na hatua ya kwanza wanatibiwa na watapona," anabainisha Dk. Mollel

Anaeleza kwa miaka mitatu Shirika la Afya Duniani (WHO), lilitegemea wastani wa vifo vya kinamama mwakani kuwa 250 kati ya vizazi hai 100,000, lakini uwekezaji wake Rais Samia, fedha shilingi trilioni 6.6, zimeshusha wastani kutokanana huduma muhimu sasa zimefika ngazi ya zahanati.

AFYA

MAGONJWA YASIYOAMBUKIZA...

# Magwiji dunia wakusanyika Dar kuumiza vichwa mapambano yake

**Na Christina Mwakangale**

• WHO: Unyanyapaa shida; TZ Iko pazuri...

NCHI zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, ikiwamo Tanzania, zinatajwa kuwa na hatari kubwa ya watu wake kuugua Magonjwa Yasiyoambukiza (NCDs), huku Shirika la Afya Duniani (WHO), linasema takriban vifo nusu milioni vinavyoepukika, hutokea kila mwaka,

Kati ya vifo hivyo 100,000 husababishwa na magonjwa manne; kisukari aina ya kwanza; selimundu; mfumo wa hewa; magonjwa ya moyo ya kuzaliwa nayo.

Tanzania imekuwa mwenyeji wa kongamano la kimataifa barani Afrika dhidi ya NCDs katika mradi 'PEN Plus' (Kifurushi cha Huduma Muhimu za Afya), kwa magonjwa hayo, lililoandaliwa na WHO, likikaribisha washiriki zaidi ya 300.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu akifungua kongamano hilo lililoanza Aprili 23 hadi 25, mwaka huu, anasema: "Nchini, NCDs huchangia takriban asilimia 70 ya magonjwa mengine kama vile figo na moyo.

"Asilimia tisa ya Watanzania wanaugua kisukari huku asilimia 15 wanaugua presha. Lengo la dunia ni kufikia angalau theluthi moja kupunguza NCDs,

"Asilimia 77 ya NCDs ipo katika nchi za uchumi kati na mdogo. Zipo hatua tunachukua kama nchi, kwa kuhimiza ufanyaji mazoezi, kutoa elimu kubadili mtindo wa maisha, kufanya vipimo na matibabu."



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, katika kongamano hilo. **PICHA: MTANDAO**

**AFRICA CDC**

Mkuu wa Kitengo cha Kudhibiti Magonjwa na Kukinga kutoka Kituo cha Kukinga na Kudhibiti Magonjwa Afrika (Africa CDC), Dk. Abdulaziz Mohammed, anaeleza:

"Afrika tunachangia masuala kadhaa na pakubwa katika NCDs, hakuna afya bila tiba ya NCDs. Unyanyapaa unatakiwa kuondolewa. Kuna watoto wanaugua kisukari aina ya kwanza. Hakuna huduma.

"Kwa kuunganisha juhudi, tutaweza kupambana na NCDs, tuachane na unyanyapaa. CDC tutaendelea kushirikiana na wadau dhidi ya NCDs Afrika."

**ATOA USHUHUDA WAKE**

Akiushuhudia umma uliohudhuria kongamano hilo, Emmanuel Kisembo, mzaliwa wa Kampala, nchini Uganda, pia Meneja wa Programu katika taasisi ya Sonia Nabeta Foundation huko kwao, anasi simulizi ya namna aligundulika kuwa ana kisukari aina ya kwanza.

"Nasimama hapa nikiwawakilisha wenzangu, mimi mwenyewe, kwa watu ambao wanaishi na kisukari. Mtoto nayegundulika na kisukari aina ya kwanza, tumesikia mawasilisho hapa yakisema, watoto hawa hawawezi hata kushehereka siku ya yao ya kuzaliwa ya kwanza.

> **Watu wengi na familia zao wanakumbana na gharama kubwa za matibabu haya au zile za usafiri kwenda na kurudi, kutoa huduma na kusababisha ulemavu ama vifo.**

"Huu ndio uhalisia. Tuna wakilisha watu ambao hufa, bila hata kugunduliwa, kutokana na uhaba wa huduma za afya. Ninawakilisha watu ambao wana familia, ambao hutumia fedha za kwa ajili ya matibabu, ada duni, nawakilisha watoto ambao wanaugua na wanashindwa kwenda masomoni.

"Tunahitaji fursa zaidi katika kuongeza wigo hali hii, wakati kwenye kongamano hili tukiwa nane, tunawawakilisha Waafrika wengi," anasema Kisembo.

Anasema kuna haja ya kutekeleza yanayopangwa na wadau mbalimbali, kwamba: "Nilifanikiwa kwenda shule, kuoa na kuwa na watoto. Hii si hadithi ya wengi waliopo huko duniani, tusirudi nyuma katika kuwafikia wengine.

"Watu wanaoishi na NCDs wanahitaji waishi miaka mingi, wakiwa na afya njema," anaongeza Kisembo.

**KUTOKA WHO**

Taasisi yake imejikita katika kupunguza gharama kubwa za matibabu kwa watoto wenye kipato cha chini wenye kisukari cha aina ya kwanza, barani Afrika.

Kisembo, ni miongoni mwa maelfu ya Waafrika, wanaoishi na kisukari aina hiyo. Anatoa elimu kwa njia tofauti. Ndiye mwandishi wa kitabu cha 'Embracing the Pricks: The Journey to Acceptance through the Lens of an African Type 1 Diabetes Warrior.'

Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Afya Duniani (WHO), nchini, Dk. Charles Sagoe-Moses, anasema NCD's, husababisha mamilioni ya vifo kwa mwaka, ambayo vingeweza kuepuka, kutokana huduma duni kukabili magonjwa hayo.

"Takriban vifo 100,000 husababishwa na sababu nne; kisukari aina ya kwanza, selimundu, magonjwa ya mfumo wa hewa na moyo kwa watoto.

"Katika nchi nyingi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, huduma za matibabu kwa NCD's hupatikana tu kwenye hospitali za rufani.

"Watu wengi na familia zao wanakumbana na gharama kubwa za matibabu haya au zile za usafiri kwenda na kurudi, kutoa huduma na kusababisha ulemavu ama vifo," anasema Dk. Charles.

Kwenye nchi hizo, anasema watoto wakigundulika kuwa na kisukari aina ya kwanza, uwezekano kwa kuishi ni kwa kipindi cha chini ya mwaka mmoja, ikilinganishwa na nchi zilizoendelea ambao uwezekano ni hadi umri wa kati.

"Kila siku watoto wa Kiafrika 1000 wenye selimundu huzaliwa. Bila ya kuwa na hydroxyurea (moja ya tiba), ambayo ni tiba iliyodumu kwa takribani muongo mmoja, nusu ya watoto hawa watafariki kutokana na ugonjwa huu kabla ya kufikishwa miaka mitano.

"Asilimia 20 ya wenye umri wa miaka tisa kwenye nchi za uchumi chini ambaye pengine angepona kwa magonjwa ya mfumo wa hewa, atafariki akiwa na miaka sita," anaeleza Dk. Charles.

Ongezeko la NCDs, mkuu huyo kutoka WHO, anasema inatia shaka, akifafanua kuna kitu kimeachwa kinapaswa kurejewa "Zamani magonjwa haya ilikuwa ni watu wazima."

**MTAFITI NCDS**

Dk. Mary Mayige, Mtafiti Mkuu Mwandamizi katika NCDs kutoka Taasisi ya Taifa ya Tafiti za Magonjwa ya Binadamu (NIMR), amejikita katika kufanya tafiti za magonjwa hayo.

Anasema magonjwa yameongezeka zaidi kuanzia miaka ya 2000, kwa kuwa idadi ya wagonjwa inathibitika kwenye hospitali.

"Kuna mpango wa serikali uliandaliwa kuyadhibiti mwaka 2008 mwaka 2016 hadi 2020 na unaondelea ulianza 2021 hadi 2026," anaeleza.

Kwa Tanzania kuwa mwenyeji wa kongamano hilo la kwanza, ni kutokana na hatua zake za kudhibiti kama vile NCDs kuingizwa katika Mpango wa Tano wa Sekta ya Afya.

Aidha, mpango wa kudhibiti NCDs ukazinduliwa, ukitekelezwa kwa afua tofauti kwa kushirikiana na taasisi za umma na binafsi.

"Juhudi zinaendelea kufanyika ila kuna changamoto ya rasilimali; fedha, watu, miundombinu nikiri kuna juhudi, huduma za kibingwa, bobezi na wengi hufika nchini kutibiwa NCDs.

"Mradi huu unafanyika kwenye nchi 11 duniani na Tanzania imeonekana kufanya vizuri zaidi, ndio mkutano wa kwanza umefanyika Tanzania, ili waje kujifunza, tumewezaje kufika hadi vituo vya afya.

"Tumeanzisha kliniki za wagonjwa NCDs na huduma za kibingwa katika wilaya mbili Karatu na Kondoa. Hadi sasa Kondoa kuna wagonjwa zaidi ya 93 na tumelenga kufikia hadi 400 kupitia mradi huu,

**MAAZIMIO YALIYOPO**

Akisoma maazimio yaliyofikiwa watekelezaji wa mradi huo kwa niaba ya Waziri wa Afya, Mkurugenzi wa Tiba Wizara ya Afya, Dk. Hamad Nyembea, anasema lengo ni kuongeza uwekezaji katika afya.

Kwamba maazimio ni bajeti ya asilimia 0.3 katika Sekta ya Afya duniani, ijikite kwenye NCDs katika nchi zinazoendelea, pia washirika wa mapambano wa magonjwa hayo kuongeza mafunzo, vifaa tiba katika maeneo ya kutoa huduma za afya.

MAZINGIRA

ZIMAMOTO & MGAMBO WA UOKOAJI...

# Serikali inavyojipanga zama mpya kukabili majanga kwa staili ngeni

**Mwandishi Wetu**

MAJANGA ya moto na ajali hadi sasa, yameendelea kutesa na kusababisha vifo, huku suluhu ya kudumu bado haijapatikana.

Matukio makubwa kuungua maduka, majengo na migahawa iliyopo Kariakoo Dar es Salaam mwaka jana na kuteketea soko la Karume Dar es Salaam mwaka juzi, yanaonyesha hali tete.

Mengine ambayo yameshatikisa nchini na kuua, ni ajali ya ndege Precision Air, iliyotokea mwaka jana mjini Bukoba, mkoani Kagera, ikaua watu 19.



Behewa la treni ya Shirika la Reli Tanzania (TRC) lililopata ajali. **PICHA: MAKTABA**

### MV SKAGIT – 2012

Ni ajali iliyotokea miezi 10 tu, baada ya ajali nyingine MV Spice Islander. Ilikuwa Julai 18, 2012 majira ya alasiri, meli MV Skagit ilipozama eneo la Chumbe, Zanzibar ikitoka Dar es Salaam, safarini kuelekea Zanzibar na watu 290, katika mgawanyo; wafanyakazi tisa melini, abiria watu wazima 250 na watoto 31.

Meli ya Skagit iliua watu 81, wakiwamo Watanzania 75; Wakenya watatu; Waholanzi wawili; Mrundi mmoja. Aidha, watu 212 walipotea ajalini na 154 walinusurika, wakiwamo; Waholanzi watano; Wajerumani wanne; Wabelgiji, Wamarekani, na Waisraeli, idadi yao wawili kwa kila utaifa.

### TRENI MSAGATI – 2002

Nayo inaingia katika rekodi ya ajali mbaya za reli nchini, ikitokea kilomita 388 kati ya stesheni za Igandu na Msagali, Dodoma Juni 24, 2002 saa 2.30 asubuhi, watu 281 walipoteza maisha.

Maiti 193 zilitambuliwa na kuchukuliwa, huku 88 walizikwa na mamlaka za serikali kwenye maziko iliyogusa halaiki katika makaburi ya Maili Mbili, Miyuji jijini Dodoma, Juni 27, 2002 kutokana na kutotambuliwa.

### MV NYERERE - 2018

Mnamo Septemba 2018, watu 224 walifariki na wengine 41 wakiokolewa, katika ajali ya kivuko cha MV Nyerere, mkoani Mwanza.

Ilikuwa ajali inayoacha kumbukumbu inayofanana na MV Bukoba iliyotokea Ziwa Victoria, Mhandisi Alphonce Charahani, akiwa wa mwisho kuokolewa, akiwa hai, baada ya kukaa majini kwa saa 48.

Rais wa wakati huo, hayati John Magufuli akaeleza kivuko cha MV Nyerere, kilikuwa na uwezo wa kubeba abiria 101, lakini kwa takwimu za miili iliyopatikana, pia manusura ni wazi chombo hicho kilibeba abiria wengi kuliko uwezo wake.

### MV BUKOBA - 1996

Inabaki kuwa ajali ya kihistoria iliyoua watu wengi zaidi kwa wakati mmoja nchini, katika miongo ya hivi karibuni. Ilitokea Mei 21, 1996, hata serikali ikakiri ajali hiyo itaendelea kuwa kumbukumbu mbaya kitaifa ya kuangamiza maisha ya mamia ya Watanzania kwa wakati mmoja.

Inakadiriwa zaidi ya watu 800 walifariki katika ajali hiyo iliyotokea kilomita 56 kutoka bandarini Mwanza. Imepita miaka 26 sasa tangu kuzama MV Bukoba, lakini kwa aliyekuwepo na asiyekuwapo, historia inaendelea kudumu kwao.

### MV SPICE ISLANDER

Kuzama meli MV Spice Islander, Septemba 10, 2011 eneo la Nungwi, Kaskazini mwa Unguja, kulileta huzuni kwa wakawzi wa mahali hapo, kukiwapo idadi kubwa ya waliofariki.

Ripoti ya jopo lililoundwa kuchunguza ajali hiyo, chini ya Jaji Abdulhakim Ameir, aliyewaongoza watu 10, inataja watu 1370 walipoteza maisha. Matokeo ya uchunguzi yanaeleza, meli ilibeba abiria idadi mara nne zaidi ya uwezo wake; ilikuwa na abiria 2,470 wakati uwezo wake ilikuwa watu 620. Ni mkasa kama huo, ndio ulipata meli MV Bukoba.

Tume iliyoundwa, inasema meli hiyo ilibainika kuwa na hitilafu iliyojulikana miezi miwili kabla ya kuzama, kupitia ukaguzi uliofanywa na Taasisi ya Usalama wa Bahari, lakini bado meli hiyo ilipewa leseni.

### FUNZO LA MAJANGA

Pamoja na kupatikana majanga mengi, inalalamikiwa bado hakuna mkakati madhubuti wa kujikinga na kujiandaa kukabiliana nayo, kama inavyotakiwa na kanuni rasmi za usafiri huo.

Mahitaji yanayotajwa ni kuwapo Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lenye uwezo, ikiwa na askari wengi, wenye vifaa vya kutoha kwa uokoaji.

Pia, kunakuwapo vikundi vya uokoaji mbalimbali vilivyoanzishwa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, vinavyopewa mafunzo mahsusim, ili kukitokea janga, navyo vishiriki kikamilifu.

Hao ni wananchi vya kujitolea wanaozisaidia sana nchi zao, mfano hai Ujerumani na Japan, wanakosaidia majanga kama ya tetemeko la ardhi, ajali za barabarani, mafuriko na majanga ya moto.

### DARASA LA UJERUMANI

Ni kawaida kuwaona wananchi wanaojitolea nchini Ujerumani, katika operesheni zote za ukoaji wa majanga. Hao ni waliopewa mafunzo maalumu ya uokoaji, wakilipwa wanalipwa na wanasaidia kupunguza madhara ya majanga.

Makundi hayo ya wanachi ya uokoaji, yanatajwa kusaidia hasa maeneo ya vijijini, ambako wanaZimamoto hawana ofisi.

Kwa mujibu wa takwimu tangu mwaka 2018, kuna watu 22,000 wanaofanya kazi ya kujitolea ya uokoaji wanaolipwa, kila wanapofanya kazi hiyo tu.

### MAONI NCHINI

Juma Waziri, ni mfanyabiashara wa Kariakoo, anayesimulia mkasa, kwamba duka lake liliungua moto, hivyo anashauri kupitia uzoefu wake, ni busara wananchi washirikishwe kupewa mafunzo ya kujikinga na kujiokoa, pale janga linapotokea.

> **“ Wananchi wanapopewa mafunzo na kushirikishwa kuokoa, kunasaidia, badala ya ilivyo sasa wanasubiri wahusika wa Zimamoto kufika, moto unakuwa umeshateketeza mali.**

Anasema, wananchi wanapopewa mafunzo na kushirikishwa kuokoa, kunasaidia, badala ya ilivyo sasa wanasubiri wahusika wa Zimamoto kufika, moto unakuwa umeshateketeza mali.

Mwenyekiti wa zamani wa chama NCCR-Mageuzi, James Mbatia, anautaja moto ni miongoni mwa majanga endelevu katika maisha ya kila siku, hivyo kunahitajika elimu stahiki ya kupambana nayo, pia majanga mengine kama hayo.

Mbatia ambaye ana taaluma ya Uhandisi Ujenzi- Mazingira, anasisitiza kunahitajika utekelezaji sheria zinazosimamia majanga, kuwalinda wafanyabiashara na majanga ya moto.

“Kwa kuwa sheria ya kuanzisha taasisi ya kupambana na kusimamia majanga ipo iliyotungwa 2015 (Disaster Management Act), serikali inabidi iipe kipaumbele utekelezaji sheria hiyo, kwa kuanzisha taasisi hiyo ya kupambana na majanga,” anasema.

### WAZIRI MASAUNI

Ni tamko lake Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Masauni, kwamba serikali inadhamiria kuboresha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, kwa ununuzi wa nyenzo mpya.

Hapo anazitaja kuwa; magari ya kuzima moto takriban 150, magari 20 ya kubeba wagonjwa, boti za kisasa 25 za na helikopta moja, zote ni maalumu za uokoaji.

Masauni akizungumza katika Mkutano wa Kuwajengea Uwezo Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala, ulioandaliwa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), anataja kuwa sehemu ya juhudi za kupambana na athari za majanga, pindi zinapotokea, ikiwamo moto.

Hapo akawaomba wakuu wa mikoa kuhakikisha kunakuwapo vituo vya kuchota maji, yatakayotumika penye majanga ya moto.

Mengine anayataja kuwa vipaumbele kwa Jeshi hilo, ni kuimarisha vitendea kazi vya zimamoto na uokoaji, ujenzi wa vituo vya zimamoto pamoja na nyumba za makazi ya askari wa jeshi hilo.

Hayo yanatokea kitaifa,ipo mifano mibaya ya moto, mwaka 1994, zaidi ya wanafunzi 40 nchini, wakapoteza maisha na mali zao.

Pia, mwaka 2009 shule ya sekondari mkoani ikateketea kwa moto, ikiripotiwa zaidi ya wanafunzi 20 walipoteza maisha.

AFYA

USALAMA MAHALI PA KAZI

# Simulizi ya utatu wa serikali, mwajiri na mwajiriwa wanavyojitwisha wajibu wao

Na Mwandishi Wetu

KILA Aprili 28 ya kila mwaka, dunia huadhimisha Siku ya Kimataifa ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi, lengo ni kuhamasisha afya na usalama wa wafanyakazi katika maeneo tofauti duniani.

Hiyo pia, ni sehemu ya haki, shukurani na madai ya wafanyakazi, katika siku yao waliosherehekea jana Mei Mosi ya kila mwaka, kama ilivyokuwa jana, kitaifa yakiadhimishwa mkoani Arusha. Siku ya Usalama Mahali pa Kazi, ni muhimu kwa taasisi zote, umma na binafsi, kwa sababu sheria za ajira inawabana ziwajibikie taratibu na kanuni zilizowekwa, pia kwa wafanyakazi ambao kwa asilimia kubwa hutumia muda mrefu kazini.

Kuwapo maadhimisho maalum ya siku hiyo, ni muhimu, kwa sababu kila mwaka, inawakumbusha na kuwahamasisha waajiri, kuboresha mazingira yao kazini, ili kuleta ufanisi na kulinda afya na usalama wa wafanyakazi wao. Afya na Usalama Mahali pa Kazi, hutofautiana kati ya sekta moja na nyingine, kutokana na aina ya shughuli zinazofanywa.

Inaelekezwa, sio kigezo kwa taasisi uzingatia zaidi baadhi ya kanuni na taratibu zilizowekwa kuliko nyingine. Zote zinapaswa kutekelezwa kisheria.



Mantiki ya namna usalama mahali pa kazi inayotekelezwa kwa vitendo. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

### DK. DOTTO BITEKO

Katika maadhimisho kitaifa jijini Arusha, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, akawataka waajiri, washirikiane na wadau kuboresha mazingira ya kazi, ili kuongeza usalama mahala kazi.

Vilevile, inaendana na kuwawezesha watumishi kufanya kazi katika mazingira rafiki, hata kukuza uzalishaji na kupunguza gharama za uzalishaji.

"Niwatake waajiri na waajiriwa, kuhakikisha usalama mahali pa kazi, mtu wa kwanza kujali usalama wake ni mwajiriwa.

"Ukiona mtambo hauko salama, toa taarifa kwa mwajiri wako; hapa hautaonekana umegoma, bali ni kuhakikisha mazingira ya kazi yanakuwa salama," anasema Dk. Biteko.

Akautaka Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA), kwa kushirikiana na wadau wa usalama kazini, wanaohakikisha wafanyakazi wanakuwa na mazingira rafiki kuwawezesha kuwa salama, furaha na matumaini wakipata ari kuendelea kufanya kazi na kuongeza ufanisi.

Anasema, pamoja na hatua zinazochukuliwa kutoa elimu, bado inahitajika kuhakikisha pande husika zinaendana na matakwa ya kitaifa na kimataifa.

Aidha, anawataka Watanzania kuhakikisha wanakuwa na mkakati wa upandaji miti na nyinginezo, kukabiliana na madhara ya tabianchi, kama vile kuhifadhi vyanzo vya maji.

> **"Tunatambua kwamba kujizatiti kwetu kwa usalama sio tu kuwalinda wafanyakazi wetu bali pia kunachangia mazingira yetu.**



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Patrobasi Katambi, anasema serikali inashirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO), kuhakikisha nchi inazingatia usalama na afya kazini.

### WANAVYONENA WADAU

Meneja wa Masuala ya Afya, Usalama, Ulinzi, na Mazingira (HSSE) wa Asasi ya Puma Energy Tanzania, Ambokege Minga, anaeleza dira ya afya ya kampuni yao ni: "Kuwezesha na kuendeleza wafanyakazi wetu kuwa mstari wa mbele katika masuala ya afya, usalama, ulinzi na mazingira, ili kuziwezesha jamii zetu.

"Hii inamaanisha kwamba tunaendelea kujitolea kila wakati kuendeleza wafanyakazi wanaohusishwa, wanaowezeshwa na wanaoshirikishwa kuweka kipaumbele kuhusu afya na usalama wao, pamoja na wa wengine.

"Kila mtu ana haki ya kuwa salama kazini na kurudi nyumbani kwa familia na marafiki akiwa na afya njema kama walivyoanza siku.

"Tunatambua kwamba kujizatiti kwetu kwa usalama sio tu kuwalinda wafanyakazi wetu bali pia kunachangia mazingira yetu," anasema.

Ambokege anaendelea: "Kampuni inaongozwa kwa mujibu wa amali ambazo zinawataka wafanyakazi na washirika wote kuzifuata katika uendeshaji shughuli zetu za kila siku.

"Tunajivunia kuwekeza nguvu kubwa katika kutoa elimu na kuwahamasisha wafanyakazi kuzingatia masuala ya afya na usalama mahali pa kazi na kuwa mabalozi kwa wenzao nchini kote.

'Tumewapatia nguvu ya kusimamia na kutoa taarifa muda na mahali popote ambapo wataona kanuni za afya na usalama zitakapokiukwa," anaongeza Minga.

Mdau huyo anaeleza, kuzingatia afya na usalama hauishii kwa wafanyakazi pekee, pia makandarasi wanaofanya nao kazi na wageni wanaowatembelea, sehemu zao za kazi.

Lengo analitaja, ni kuhakikisha hakuna anayeumia au kupata madhara, pindi anapofanya nao kazi.

Asasi hiyo inafafanua kwamba, katika juhudi zake inatoa vifaa vya kuwakinga na hatari zinazoweza kujitokeza mahali pa kazi, kama vile vikinga mwili. Pia, asasi hiyo inawahamisha kutoa taarifa, wanapoona sheria zinakiukwa. Kwa mfano, wanapoona mkandarasi anafanya kazi akiwa amevalia vikingamwili, lakini wafanyakazi wake hawana.

"Hii inaenda sambamba na kuwatia moyo kutoa taarifa kwa matukio ambayo si salama katika utendaji wa kazi. Matukio haya hutoa mafunzo na elimu kwa wafanyakazi wote ili kudhibiti kutojirudia," anasema na kuongeza:

"Tunajivunia kuwa mpaka sasa tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa kufikia malengo makubwa ya masuala ya afya na usalama, kwa sababu hatujapata kesi za ajali au vifo mahali pa kazi, kuanzia mwaka, mpaka sasa hivi.

"Tunafanya jitihada kubwa katika kutoa elimu, kuwalinda na kuwahamasisha wafanyakazi wetu wote katika shughuli zetu za upokeaji, utunzaji na usafirishaji wa mafuta kwa maendeleo ya wananchi na taifa zima kwa ujumla," anasema Minga.

Mtaalamu wa Udhibiti wa Mazingira ya Usalama wa Afya na Ubora wa kampuni hiyo, Rehema Madoffe, anaeleza kuwa: "Tunahakikisha wafanyakazi wote wanakuwa na bima za afya bora, ambazo huwalinda pindi wanapokumbwa na changamoto za kiafya.

"Pia, mahali pa kazi kuna miundombinu imejengwa kwa uthabiti na ubora ili kukabiliana na changamoto mbalimbali kama vile majanga ya moto.

"Kwa kuongezea, wafanyakazi hupatiwa mafunzo kukabiliana na majanga ya moto ambapo kila mwezi kwa baadhi ya maeneo yetu ya kazi huwa tunafanya mafunzo ili kujiandaa pindi tunapokumbwa na majanga ya aina yoyote." amesema.

Maadhimisho ya mwaka huu, 2024 yameongozwa na kaulimbiu 'Kuangazia Athari za Mabadiliko ya Tabianchi kwa Usalama na Afya Kazini'.

Kwa mujibu wa ILO), kaulimbiu hiyo inatokana na uhalisia wa mabadiliko ya tabianchi duniani, yanayoathiri wafanyakazi, kupitia hatari zinazoongezeka, kama vile joto kali, mionzi, mabadiliko ya hali ya hewa, uchafuzi wa hali ya hewa na magonjwa yanayosababishwa na mionzi.



# Bashe aibana Bodi ya Mkonge

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe ameagiza Bodi ya Mkonge nchini kupitia upya mfumo wa masoko wa kuuza katani ili mkulima apate soko la uhakika lenye maslahi.

Bashe alitoa kauli hiyo wakati akizindua Bodi mpya ya Wakurugenzi jijini hapa.

Alisema: "Bodi ya Mkonge haitakiwi kukaa Tanga, Dar es Salaam na Dodoma, mnatakiwa kwenda kutafuta masoko ya kimataifa na nitawapima kupitia namna mtakavyoimarisha mfumo wa masoko."

Alisisitiza bodi hiyo kuhakikisha inaandaa miundombinu rafiki itakayowezesha kuongeza tija kwa zao hilo huku akihimiza wafanye kazi kwa bidii na kuwasaidia wakulima wa zao hilo.

Mwenyekiti aliyemaliza muda wake, Mariamu Nkumbi, alisema katika kipindi cha uongozi wao wamefanikiwa kurejesha mali za bodi kama jengo, wamekarabati majengo, idadi ya wafanyakazi imeongezeka.

Pia, alisema fedha zimeongezeka, wamehamasisha zao la Mkonge katika mikoa 13, wamesambaza mbegu katika wilaya 16.

"Hivi karibuni kuna mikoa itaanza kulima mkonge. Mafanikio tuliyapata ni pamoja na jengo la mkonge kurudishwa baada ya kubinafsishwa. Tumefanikiwa pia kurejesha baadhi ya nyumba," alisema Nkumbi.

Mwenyekiti mpya wa bodi hiyo, Theobald Thabi, aliahidi kushirikiana na wenzake kutatua changamoto zilizopo.



Mbunge wa Pandani Zanzibar, Maryam Omary Said, akipokea zawadi ya fulana kutoka kwa Mkurugenzi wa Shirika la Akili Platform Tanzania (APT), Roghat Robert, wakati viongozi wa shirika hilo, walipotembelea bungeni Dodoma, mapema wiki hii. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Marufuku kucheza 'Pool' asubuhi

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

MKUU wa Wilaya ya Mkalama mkoani Singida, Moses Machali, amepiga marufuku mchezo wa 'Pool Table' nyakati za asubuhi na kuonya kuwa atakayekiuka amri hiyo atachukuliwa hatua za kisheria.

Machali alitoa amri hiyo wakati akizungumza na wakazi wa vijiji vya Senene na Lukomo vilivyopo Kata ya Iguguno ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kikazi ya kusikiliza na kutatua kero zinazowakabili wananchi.

"Vijana waende wakafanye kazi, marufuku mchezo ya Pool Table asubuhi, wazazi kaeni na vijana wenu, wafundisheni maadili, wasiwe na haraka ya kufanikiwa maisha kwa njia zisizo halali," alisema.

Kwa upande mwingine, Machali alitoa muda wa mwezi mmoja kwa watendaji wa vijiji, kata na walimu wakuu wa shule kuhakikisha wanatatua tatizo la uhaba wa madawati katika shule zote zilizopo wilayani hapa.

"Natoa kipindi cha mwezi mmoja kwa watendaji wa vijiji, kata, walimu wakuu shule za msingi na sekondari kuhakikisha tatizo hili la madawati linakwisha," alisema.

Vilevile, Machali alipiga marufuku ukodishaji wa mashamba ya shule badala yake yatumike kulima chakula kwa ajili ya wanafunzi.

"Ardhi ya shule isikodishwe kwa mtu yeyote ile, limeni chakula kwa ajili ya watoto wa shule, nisisikie hata mwalimu anajikodisha shamba la shule," alisema.

# Gondwe ataka ushirikiano ulinzi

**Na Mwandishi Wetu,** SINGIDA

MKUU wa Wilaya ya Singida, Godwin Gondwe, amesema wamiliki wa kampuni za ulinzi wanapaswa kushirikiana na vyombo vya usalama vya serikali ili kuimarisha usalama wilayani hapa.

Akizungumza katika kikao cha pamoja na wamiliki hao, alisema kampuni hizo zinapaswa kuzingatia maadili ya kazi za usalama katika malindo waliyokabidhiwa.

"Nataka kuona mnajenga utaratibu wa kuzungukia malindo yenu ili kujua kinachoendelea... hakikisheni walinzi wenu wanazingatia maadili ya kazi," alisema.

Gondwe aliwashauri wamiliki hao kuajiri walinzi waliopitia mafunzo ya ulinzi na usalama kupitia Jeshi la Akiba kwani yanawafanya kuwa wakakamavu na mbinu za ulinzi.

Alisema ofisi yake inaratibu kanzidata ya wahitimu wa jeshi hilo, hivyo wamiliki hao wawasilishe maombi kwa ajili ya kupata vijana waliohitimu wenye umri stahiki kwa kazi hizo.

Kuhusiana na malalamiko ya baadhi ya kampuni kutolipwa fedha zao za ulinzi, Gondwe alizitaka kujiorodhesha na kuwasilisha kwake orodha ya wadaiwa na kuhakikisha kila mmiliki anakuwa na mikataba mizuri ili kuepuka kupoteza haki zao.

# Walimu waagizwa kufuatilia wanafunzi

**Na Mwandishi Wetu,** SINGIDA

OFISA Elimu wa Mkoa wa Singida, Dk. Elipidius Baganda, amewaagiza walimu mkoani hapa kufundisha kwa malengo na kufuatilia maendeleo ya wanafunzi kitaaluma ili kuongeza kiwango cha ufaulu.

Akizungumza kwenye kikao kazi cha tathmini ya mitihani ya taifa, Baganda alisema kuwa: "Fanyeni kazi kwa malengo na ufuatiliaji, malengo ni yale ambayo nilisema la nne kufaulu wote la saba asilimia 85, kidato cha pili wafaulu wote cha nne ufaulu kuanzia asilimia 50 na kidato cha sita wafaulu kwa asilimia 100."

Alisisitiza suala la nidhamu kwa walimu na wanafunzi lizingatiwe na kwamba wanafunzi wapatiwe mazoezi ya kutosha na ya sahihishwe na maswali yanayotungwa yazingatie viwango.

# REA kusambaza umeme vitongoji 31,532

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKALA wa Nishati Vijijini (REA) umejipanga kusambaza huduma ya umeme kwenye vitongoji 31,532 vilivyobaki nchini, ili kuharakisha upatikanaji wa huduma hiyo na kuboresha hali ya maisha ya wananchi wa vijijini.

Mkurugenzi Mkuu wa REA, Hassan Saidy alitoa takwimu hizo juzi alipokuwa akitoa wasilisho kuhusu mpango wa kuharakisha upelekaji wa umeme katika vitongoji vya Tanzania Bara.

Alisema ili kufikisha huduma ya umeme kwenye vitongoji hivyo kunahitajika kujengwa njia za umeme wa msongo wa kati zenye urefu wa kilomita 41,593 na kilomita 87,206 za msongo mdogo, kufunga mashine umba 31,532 na kuunganisha wateja wa awali 1,552,343 ambapo mradi huo utagharimu Sh. trilioni 6.7.

Saidy aliwaeleza wabunge kuwa kuanzia mwaka 2008 hadi mwaka 2020 REA wamekamilisha miradi mikubwa ya gridi ya taifa 15 na inaendelea na utekelezaji wa miradi mikubwa saba ya kupeleka umeme vijijini iliyoanzishwa katika kipindi cha mwaka 2021.

"Baada ya kukamilika kwa miradi hiyo saba, jumla ya vitongoji 9,480 na wateja wa awali 534,906 wataunganishwa na huduma za umeme kupitia ujenzi wa kilomita 26,379 za njia za umeme msongo wa kati na kilomita 26,145 za njia ya msongo mdogo, pamoja na usimikaji wa mashine umba 9,161 kwa gharama ya Sh.trilioni 2.3," alisema.

Aliongeza kuwa lengo la kuanzishwa kwa REA wakati huo lilikuwa ni kuharakisha upatikanaji wa huduma za nishati bora vijijini kwa madhumuni ya kuboresha hali ya maisha ya wananchi wa vijijini, kuchangia ipasavyo katika ukuaji wa uchumi, kuboresha huduma za jamii, kuhifadhi mazingira na kuimarisha usawa wa kijinsia na hali ya upatikanaji wa umeme.



# TAKUKURU yaagiza kuchukuliwa hatua wanaokwamisha miradi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKURUGENZI wa Halmashauri mkoani Njombe, wametakiwa kuchukua hatua kali za kisheria kwa wale wanaohusika kufanya uzembe ikiwemo kukwamisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayoletwa na serikali.

Kauli hiyo ilitolewa na Kamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Njombe, Kassim Ephrem wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Alisema mkurugenzi anapopelekewa ripoti ya mradi uliotembelewa na TAKUKURU na kubaini upungufu wanategemea kuona mkurugenzi anachukua hatua kwani upo uwezekano wa kupewa taarifa za uongo na mhandisi anayemuamini.

"Mkurugenzi mradi upo kwenye eneo lako tumeenda TAKUKURU tumekuletea barua tekeleza basi haraka ili mradi uonekane, muite mhandisi wako ili kama anakulisha matangopori uone TAKUKURU wamenisaidia kwa kunipa taarifa hii," alisema Ephrem.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kuzuia miradi hiyo isiwe na upungufu mkubwa yatakayosababisha hasara kwa serikali ambayo lengo lake ni kusogeza huduma kwa wananchi.

Ephrem alisema sehemu nyingine ambayo wamebaini ni wahandisi kutotembelea miradi mara kwa mara ambapo hiyo inachangia miradi kutojengwa kwa viwango vinavyotakiwa.

"Wahandisi jengeni tabia ya kutembelea miradi ya halmashauri na ile mingine ya serikali ili utoe maelekezo pale unapoona kuna upungufu ili kama kuna malalamiko yoyote upeleke kwa mkurugenzi ili atatue changamoto iliyojitokeza," alisema Ephrem.

Alibainisha kwamba taasisi hiyo kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia Januari hadi Machi mwaka huu jumla ya miradi 21 imefuatiliwa yenye thamani ya Sh.bilioni 7.3.

Alisema katika miradi hiyo sita ambayo thamani yake ni Sh. bilioni 4.4 imebainika kuwa na upungufu mbalimbali ambayo wameagiza yafanyiwe kazi.

Hata hivyo aliwakumbusha wanachama wa vyama vya siasa kufuata miiko na maadili ya vyama vyao kwa kuepuka vitendo vya rushwa kwenye uchaguzi.

Alisema wapo baadhi ya wanachama wanaanza kufanya vitendo ambavyo si vya kimaadili na miiko ya vyama vyao.



Wakazi wa Mitaa ya Majengo Mapya na Igamba, Kata ya Nsalaga, jijini Mbeya, wakishiriki kukarabati barabara juzi, baada ya kuharibika kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha nchini. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Tindikali ya chini katika udongo chanzo uzalishaji mdogo

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MIKOA yenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula ikiwemo ya Nyanda za Juu Kusini, imetajwa kuwa na udongo wenye tindikali ya chini, hali inayosababisha wakulima watumie gharama kubwa kwenye uzalishaji na wasipate tija.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Idara ya Masoko na Mauzo wa kampuni ya mbolea ya Minjingu, Dk. Mshindo Msola kwenye mafunzo kuhusu usimamizi wa rutuba ya udongo na matumizi bora ya mbolea kwa mawakala wa pembejeo za kilimo kutoka mikoa ya Njombe, Morogoro, Iringa,na Ruvuma yaliyofanyika mjini Makambako.

Alisema kutokana na mikoa hiyo kuwa na udongo wenye tindikali ya chini wakulima wanatakiwa kutumia chokaa kilimo ili kukabiliana na hali hiyo.

Dk. Msola alisema kutokana na changamoto hiyo serikali kupitia wizara ya kilimo licha ya kutoa mbolea za ruzuku pia inatakiwa kutoa ruzuku ya chokaa kilimo ili kuwawezesha wakulima kuboresha hali ya udongo ambao utawasaidia wazalishe kwa tija.

"Kwenye mikoa mingi yenye uwezo wa kuzalisha nyanda za juu kusini milimani, Kanda ya Ziwa, upande wa Kigoma baadhi ya maeneo upande wa Kilimanjaro udongo unatindikali ya chini ya 5.5 sasa madhara yake ukishakuwa na udongo wa tindikali hii ni lazima uutibu," alisema Dk. Msola.

Dk. Msola alisema kuwa tindikali ikiwa ya chini maana yake kuna madini ambayo yako kwa wingi ambayo yanaitwa aluminium na chuma. "Madini haya ni kama minyoo kwenye ardhi kwa hiyo kadri unavyoweka mbolea inakamata yenyewe na mbolea haipatikani kwa hiyo ushauri wangu kwanza wakulima washauriwe watumie chokaa kilimo ambayo itawasaidia na mashamba mengi yatafufuka," alisema Dk. Msola.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka alitoa rai kwa maofisa kilimo kutumia utafiti huo kuona namna ya kukabiliana na changamoto ya udongo kuwa na tindikali ya chini ili kuhakikisha kutatua changamoto hiyo na kuwasaidia wakulima wazalishe mazao bora.

Baadhi ya mawakala wa pembejeo za kilimo akiwemo Lesa Mbilinyi alisema watahakikisha wanatoa elimu kwa wakulima juu ya matumizi sahihi ya pembejeo hasa mbolea na mbegu ili wazalishe kwa tija.

Awali akizungumza katika mafunzo hayo Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa alisema iko haja ya kuboresha ardhi ili wakulima wazalishe kwa tija na wameiomba serikali kuona namna ya kupunguza gharama za chokaa kilimo.

# Mradi wa REGROW wainua kiuchumi wanawake vijijini

**Na Mwandishi Wetu,** MBARALI

SERIKALI inaendelea kuwainua kiuchumi Watanzania hususani wanawake waishio vijijini kupitia miradi mbalimbali ukiwemo wa Kuboresha Usimamizi wa Maliasili na Kukuza Utalii Kusini mwa Tanzania (REGROW).

Mradi huo ambao unatekelezwa na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa lengo la kuendeleza utalii Kusini mwa Tanzania, umewainua kiuchumi wanawake kutoka vijiji vinanvyopakana na Hifadhi ya ya Ruaha, Udzungwa, Mikumi na Nyerere.

Wakizungumza na waandishi wa habari hivi karibuni, wanawake walionufaika na mradi huo kutoka katika vijiji vinavyozunguka hifadhi hizo walisema kwa sasa maisha yao yameimarika kwani wameweza kuanzisha biashara zinazo wapatia kipato cha uhakika.

Mwamvita James kutoka Kijiji cha Madibira Mkoa wa Mbeya, alisema kabla ya mradi maisha yake yalikuwa ya kugangaiza lakini kwa sasa anavuna magunia zaidi ya mia moja.

Alisema hali hiyo imemsaidia kujenga nyumba, kufungua biashara ya ushonaji iliyotoa ajira kwa wengine, huku akitoa wito kwa watu wengineo kutumia fursa zinazojitokeza katika maeneo yao.

Katibu wa kikundi cha Kordun kutoka jamii ya wamasai katika Kijiji cha Tungamalenga, Janeth Matambile alisema fedha walizopatiwa zimewasaidia kukopeshana na kuendeleza miradi mbalimbali waliyoianzisha ikiwemo unenepeshaji wa ng'ombe.

"Tulipatiwa fedha mbegu ambazo zimetusaidia kujenga mabanda ya ng'ombe ya kisasa kwa lengo la kuwanenepesha, mradi wa REGROW pia umetusaidia kuondokana na dhana potofu kuwa wanawake ni wa kukaa nyumbani tu na kwa sasa wanawake wanajishughulisha katika usindikaji wa maziwa na kutengeneza sanaa," alisema Matambile.

Katibu Msaidizi wa kikundi cha Amani kilichopo Wilaya ya Chamwino Mkoani Dodoma, Upendo Vuliva alisema mradi ya REGROW umeimarisha upendo na furaha kwenye familia kwa kuwa inawawezesha wanawake kuchangia katika pato la familia.

Msimamizi wa mradi huo, Dk. Aenea Saanya alisema kwenye utekelezaji wa kipengele cha tatu, wanawake 127 kutoka kata ya Madibira na Miyombweni waliajiriwa katika mradi wa uboreshaji wa skimu ya umwagiliaji.

"Wanawake 10 kutoka vijiji vya Uturo, Gonakuvagogolo, Matebete, Chosi na Herman, Isele, Njombe, Mbuyuni, Makangalawe, Igumbilo/Isitu na Madibira wameajiriwa katika ujenzi unaondelea wa ofisi za Jumuiya za Watumia Maji," alisema Dk. Saanya.

Dk. Saanya alisema hadi Februari mwaka huu mradi wa REGROW umewafikia wanawake 9,386 sawa na asilimia 56 ya wanufaika wote 16,872.

Kwa mujibu wa taarifa maalumu juu ya ushiriki wa wanawake katika mradi huo, hadi kufikia Februari 2024, mtaji wa vikundi vya COCOBA umekuwa ukiongezeka kwa wastani wa asilimia nne kwa mwezi kutoka Sh. milioni 61.3 Januari mwaka jana hadi Sh. bilioni 1.3 Januari mwaka huu huku idadi ya wanachama wanaostahili kupata mikopo kuongeza kutoka 483 hadi 3,496.

Aidha, wanawake 1,182 wameweza kuanzisha shughuli mpya za kujiongezea kipato, 1,814 wamewezeshwa kuboresha biashara au miradi yao na 1,859 wamewezeshwa kuboresha tija katika kilimo.

Aidha, katika uendeshaji wa mradi, asilimia 36 ya wafanyakazi ni wanawake ambao wapo katika taasisi zote.

# Mwinyi 'afagilia' uchumi wa buluu

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema Zanzibar inajengwa na sera kuu ya uchumi wa Buluu katika kuimarisha uchumi wa watu wake.

Dk. Mwinyi alisema kuwa uchumi wa buluu unajipambanua kwenye maeneo ya utalii, uvuvi na ufugaji wa vifaranga vya samaki, Bandari, mafuta, gesi na sekta ya usafirishaji wa majini.

Aliyasema hayo Ikulu, Zanzibar wakati akizungumza na Mkuu wa Chuo cha Ulinzi cha Taifa (NDC), Meja Jenerali Wilbert Augustin Ibuge na ujumbe alioongozana nao wa wanafunzi 52 wa chuo hicho kutoka mataifa 15 ya Afrika ikiwemo Tanzania na watumishi wengine wa Serikali waliofika hapo kumtembelea.

Rais Mwinyi alisema utalii wa Zanzibar ni tegemeo kwa uchumi wa nchi kwa kuwa unachangia asilimia 30 ya pato la taifa na unajumuisha utalii wa fukwe, urithi, michezo na utalii mpya wa afya na mikutano.

Kuhusu sekta ya uvuvi na ufugaji wa samaki, alisema ina fursa nyingi kwa wavuvi na ajira za mtu mmoja mmoja kwa kutumia maboti na majahazi na kilimo cha mwani kilichobeba asilimia kubwa ya wanawake.

Alisema Zanzibar inanufaika na sekta ya bandari zikiwemo bandari jumuishi ya Mangapwani ambayo kwa sasa iko kwenye matengenezo, Bandari ya Malindi, Mkokotoni na ya Fumba kwa usafirishaji, usambazaji wa bidhaa kutoa huduma na kufanyia biashara ya kupokelea mizigo, kusafirishia mazao, mafuta, nafaka na kukuza uchumi wa nchi.

Alisema, sekta hiyo inaimarisha biashara na uchumi kupitia bandari za Zanzibar, Pemba, Tanga, Dar es Salaam na Mtwara kwenda Msumbiji, visiwa vya Comoro na kwingineko.

Meja Jenerali Ibuge, alisema lengo la ziara yao ni kuimarisha biashara na usalama kwa uchumi endelevu wa Buluu Zanzibar.

# Afya ya akili tishio kwa vijana, watoto Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imesema kuna ongezeko kubwa la idadi ya watu wanaougua afya ya akili visiwani hapa wanaokadiriwa kufikia zaidi ya 5,000, wengi wao wakiwa vijana na watoto. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 Zanzibar ina idadi ya watu 1,889,773

Akizungumza jana na waandishi wa habari visiwani hapa, Mratibu wa Afya ya Akili wa Wizara ya Afya, Suleiman Abdu Ali, alisema kuwa takwimu hizo zimepatikana katika vituo vya afya ambako wagonjwa hao wamepata matibabu.

Ali, alisema Hospitali ya Wagonjwa wa Akili Kidongochekundu hupokea wastani wa wagonjwa wapya 100 hadi 150 kwa mwezi wengi wao wakiwa ni vijana na watoto.

Alisema kwa mwaka 2021, wamepokea wagonjwa 132 na mwaka 2023 wagonjwa wapya walikuwa 1,039.

"Kupatikana kwa takwimu sahihi ni changamoto kwa sababu hakuna mfumo rasmi unaoonyesha juu ya ukusanyaji wa data kwa ugonjwa huo yawezekana ikawa idadi ni kubwa zaidi," alisema.

Alizitaja sababu za kuongezeka kwa wagonjwa wa akili kwa vijana kuwa ni matumizi ya dawa za kulevya, msongo wa mawazo na kuvunjika kwa mahusiano ya kimapenzi. Ali alisema jamii imepata mwamko wa kuwafikisha hospitali wagonjwa hao ikinganishwa na miaka ya nyuma.

Mwenyekiti wa Baraza la Wauguzi na Wakunga Zanzibar, Sharifa Awadhi Salum, alisema katika kuadhimisha siku ya wauguzi na wakunga, wanaendelea kutoa elimu ya ugonjwa wa saratani na umuhimu wa chanjo ya saratani ya shingo ya kizazi kwa wasichana.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman (wa tatu kulia), akipokea sadaka ya tende kutoka kwa Balozi wa Saudia nchini, iliyotolewa na taasisi ya misaada ya kibinadamu ya mfalme Salman wa Saudia Arabia, huko Sheria House Mazizini, Mjini Zanzibar mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampuni yaamriwa kudhibiti msongamano Mnazi Mmoja

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla ametoa mwezi mmoja kwa uongozi wa Kampuni ya Lancet kitengo cha wagonjwa wa uangalizi maalum (ICU) katika Hospitali ya Wilaya ya Magharibi ' ya Mwanakwerekwe kutoa huduma ili kudhibiti ongezeko la wagonjwa Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Abdulla alitoa amri hiyo jana baada ya kukagua maendeleo ya utoaji na upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi katika hospitali hizo zilizopo Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema Lancet ina wajibu wa kuhakikisha huduma zote muhimu zinapatikana kwa ubora na haraka kwa wagonjwa wanaofika hospitali zote za wilaya ili kuondoa msongamano wa wagonjwa Mnazi Mmoja.

Alisema Serikali imelipa kipaumbele suala la kuboresha miundombinu ya afya ili kuzidi kutoa huduma bora za matibabu kwa wananchi.

Makamu huyo wa rais, aliwataka madaktari kuzingatia nidhamu, miiko, miongozo na maadili ya kazi zao na kuachana na tabia ya kuwatolea lugha chafu wagonjwa hasa wa dharura, lasivyo hatua kali zitachukuliwa kwa kwa atakayekiuka. Mkurugenzi Mtendaji wa Mnazi Mmoja, Dk. Muhiddin Abdi Mahmoud, alisema hospitali hiyo imeamua kusomesha wafanyakazi ili kukabiliana na upungufu wa madaktari na kutoa huduma bora na kwa wakati kwa wananchi.

Alisema Wizara ya Afya imeandaa utaratibu wa kuwashauri na kuwashawishi wanafunzi wanaojiunga na vyuo vikuu kusomea kozi ambazo zina uhaba wa wataalamu ikiwemo ICU, ganzi na usingizi na huduma za dharura.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**HANIFA HARUNA HASHIM** anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index **No. NS5033/0036/2014** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KONDOA ISLAMIC SECONDARY SCHOOL** mwaka 2017, Cheti hiki kimepotea mkoani Dodoma. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/15405/2024**


---

**AMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya MASWA.**
**Kituo cha NYALIKUNGU mkoa wa SIMIYU**
**Shauri la Madai Na.37/2024**
**Jins la Mdai BIOSUSTAIN SINGIDA Co L.T.D**
**Jina la Mdaiwa MANGALU GOLOMONDO**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA.**

**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa MANGALU GOLOMONDO WA NKINDWABIYE-BARIADI**
**K.K: AFISA MTENDAJI WA KIJIJI CHA NKINDWABIYE BARIADI.**
**K.K HAKIMU MKAZI MFAWIDHI**

MAHAKAMA YA MWANZO NKOLOLO Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba(Eleza hapa habari za Madai) ANAKUDAI PESA KIASI CHA SHILINGI 13,528,560/=BAKI YA PESA ZA UNUNUZI WA PAMBA. Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 02 Mwezi 05 Mwaka 2024 saa 2;00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea. ANGALIZO:Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa sharini .Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo. Hati hii Imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 18 Mwezi 04 Mwaka 2024.





---

**FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 6672 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE JANE WILFRED MWAKALEBELA**
**AND**
**In the matter of Application for Letters of Administration by**
**FREDRICK MWAKALEBELA AND LILIAN MWAKALEBELA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate or (letters of Administration) is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 9 day of May, 2023. 11:30am
Dated at DAR ES SALAAM this 2nd day of April, 2024.





---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 6794 OF 2024**
**In the matter of the late**
**MAUBE SALATIELI NYAGALU**
**AND**
**IN THE MATTER ON AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**JULIANA JOHN PETRO**

**GENERAL CITATION**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above- named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 06 Day of 05, 2024
Presented for filling this 22 Day of 4, 2024.




---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SILIVESTER PETER RUYOBYA**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA RAV 4 yenye usajili namba T 402 EDB. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA:**
**PHQ/DAR/KIN/71757/2024**

---

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**DICKSON SILIVESTER PETER**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA VITS yenye usajili namba T 402 DXD na NISSAN DUALS yenye usajili namba T 127 ECF. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA:**
**PHQ/DAR/KIN/71753/2024**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GEOFREY MJUNI BENDANTABONA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA RAV 4 yenye usajili namba T 685 CUZ. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**PHQ/DAR/UBU/75068/2024**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ROBSON GODIAS LYIMO**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NO YA USAJILI T198 AUL CHASSIS NO EE1115065383 ENGINE NO: 4E2440276 YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI

**PHQ/ARU/ARU/ 12747/2024.**

---

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA MBEYA**
**SHAURI NO.24/2024**
**NIKU EDSON:::::::::::MDAI**
**DHIDI YA**
**1.ASHA JUMA:::::::::::::::MDAIWA**
**2.ATHUMANI SAID:::::::::MDAIWA**

**YAH:KUITWA SHAURINI**
**KWA:ATHUMAN SAID**

Fahamu kwamba NIKU EDSON amefungua shauri dhidi yenu katika baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa tarehe 06/05/2024 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh.T.Munzerere Mwenyekiti wa Baraza.Mnatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Mnaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za Baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.
Kumbuka:Msipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo nyie kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe 22/04/2024.

**T.Munzerere**
**MWENYEKITI**
**22/04/2024**

---

**COURT BROKER & PROCESS SERVER**
**FAGIO BROKERS & AUCTIONEERSCO.LTD**
**P.O.BOX 1011 – MBEYA**
**MOBILE: 0786 606 041/ 075707270741**
**E-MAIL: hopembeya@yahoo.com**

**KWA,**
**A.V.M DILLGHAM CONSTRUCTION (OZUGR AYIDIN)**
**MDAI NAMBA 22/2024**
**MAHAKAMA YA MWANZO KYELA MJINI**
**MDAI: K.W SECURITY COMPANY LTD**
**(PHILIPO SALION KIWIKE)**
**DHIDI YA**
**MDAIWA:::::::: A.V.M DILLGHAM CONSTRUCTION (OZUGR AYIDIN)**
**YAH: NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14)**
**KULIPA DENI LA SHAURI HILI**

Tafadhali rejea somo la hapo juu.
Kwa amri ya mahakama, ninakupa siku kumi nan ne kuanzia tarehe ya notisi hii uwe umelipa deni la shauri hili, kamisheni ya Dalali wa Mahakama pamoja na gharama nyingine zitakazojitokeza.
Kushindwa kutekeleza hilo, hatua za ukamatji mali itafuata bila taarifa nyingine kwako.




---

**KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTE KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.**
**TUPIGIE: +255 - 0677020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**

**OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industrial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 0677020701**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**Website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Waasi M23 wauteka mji wenye madini

**GOMA,** DRC

WAASI wa M23 wameuteka mji wa Rubaya wenye umaarufu wa kuwa na migodi mikubwa ya madini baada ya kuwepo kwa mapigano makali na jeshi la serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Mapigano hayo yalianza juzi asubuhi na taarifa kutoka eneo hilo zinaeleza waasi hao wanaodaiwa kufadhiliwa na Rwanda, walifanikiwa kusukuma nyuma jeshi la serikali na kusababisha wakazi wa mji huo kukimbia mji wa Rubaya wenye migodi mikubwa ya madini huko wilayani Masisi karibu na mji mkuu wa Kivu Kaskazini mwa Goma.

Milio ya mizinga ilisikika mchana kutwa wa juzi katika mji huo, waasi wa M23 walikuwa wakizilenga kwa makombora ngome za jeshi la serikali ambalo halikufaulu kuwazuia. Baadhi ya raia wa mji huo walisema wana wasiwasi kufuatia ukimya wa kikosi cha nchi za jumuiya ya maendeleo kusini mwa Afrika, SADC ambacho hadi sasa kimeshindwa kukabiliana na waasi hao.

"Ni kweli kabisa mji wa Rubaya umedhibitiwa na waasi wa M23 tangu juzi Jumanne, kwetu ni mshangao kwasababu licha ya kuwepo kwa jeshi la SADC waasi wanasonga mbele na bila kuwazuia na hata kukabiliana nao", alisema mkazi wa Rubaya ambaye hakutaka kutajwa jina lake.

Kwa mujibu wa asasi za kiraia, udhibiti wa mji wa Rubaya umekuwa ni tukio baya kwa jeshi la serikali ya DRC ambalo hadi jana halijatoa taarifa kuhusu kuchukuliwa kwa mji huo wa kimkakati.

Ofisa mkuu kutoka muungano wa mashirika ya kiraia mkoani Kivu Kaskazini alisema amepoteza matumaini yake kwa kupatikana amani katika eneo hilo.

"Rubaya ni mji wa madini na ulimwengu mzima unategemea hapo, kwa hiyo jinsi waasi walivyouchukuwa mji huo sisi tumepoteza matumaini. Tunalo jeshi lenye nguvu lakini tatizo ni kwamba limekosa msaada," alisema Katabazi.

Aliongeza kwa kuwasihi viongozi kuchukua hatua za haraka za kutafuta mbinu mbadala ili kurejesha utulivu.

Ilielezwa kuwa mpaka jana jioni mamia ya raia wa mji huo waliendelea kukimbilia msituni huku wengine wakijikuta wakinasa majumbani mwao kutokana na milio ya risasi inayosikika kwenye milima inayouzunguka mji huo.

Kwa miezi kadhaa, waasi wa M23 walikuwa wakijaribu bila mafanikio kuudhibiti mji huo wenye madini, huku viongozi wa mashirika ya kiraia wakishutumu uuzaji haramu wa madini unaofanywa na vijana wapiganaji wanaoitwa wazalendo.

Haya yanajiri miezi minne baada ya kupelekwa kwa kikosi cha SADC ambacho hadi sasa hakijaanzisha mashambulizi ya ardini dhidi ya kundi la M23 linalouweka mji wa Goma kwenye hali ya wasiwasi. **DW**

## Museveni ampigia debe mtoto wake

**KAMPALA,** Uganda

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni, kwa mara ya kwanza amejitokeza hadharani na kumpigia debe mtoto wake ambaye ni mkuu wa majeshi ya nchi hiyo, Jenerali Muhoozi Kainerugaba, akimtaja kama mzalendo na mwenye nia ya kuboresha jeshi.

Kauli hiyo ambayo imetafsiriwa kama tangazo la kumrithi, ameitoa juzi kwenye sherehe za kumbukizi ya miaka 50 ya kuzaliwa kwa Jenerali Muhoozi.

Rais Museveni wakati akimpongeza mtoto wake alimsifu kuwa ni mzalendo na shujaa anayependa kuboresha jeshi la Uganda licha ya kuwepo kwa ukosoaji kutoka ndani na nje ya utawala wake.

"Watu wamekuwa wakimsema sana Muhoozi... Muhoozi hiki, Muhoozi hili... Aliporudi kutoka mafunzo ya kijeshi, alichangia kuboresha jeshi letu kwa sababu yeye anazingatia uzalendo na maslahi ya wanajeshi wala si kazi au utajiri. Kutokana na hayo wanajeshi wengi Afrika hupotoka," alisema Museveni.

Kiongozi hiyo ni mara yake ya kwanza kumzungumzia mtoto wake hadharani na kuuweka mtazamo wake chanya kuhusu mwanawe kujiunga na jeshi na siasa.

Miezi kadhaa iliyopita Rais Museveni alimkaripia mwanawe huyo kutokana na tabia yake ya kusambaza ujumbe usiostahili kwenye ukurasa wake wa X (zamani Twitter) hasa pale alipoandika kwamba angeivamia Kenya.

Wadadisi wa masuala ya kisiasa, walisema kiongozi huyo sasa amedhihirisha kuwa anamwamini sana mwanawe katika mazingira ya kisiasa na utawala.

Mmoja wa wadadisi hao wa kisiasa na kijeshi jijini Kampala, Wambete Wamoto, aliiambia DW kwamba Rais Museveni anawahofia majenerali wengine ambao hawakubaliani na maamuzi yake na ndiyo maana anahisi kupata kitulizo kwa mwanawe akiwa mkuu wa majeshi yote. **DW**




**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI**
**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI**

**TANGAZO LA KOZI YA UKARABATI NA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVU KAZI 'LBT'**

**1. UTANGULIZI:**
Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi "Institute of Construction Technology (ICoT)" ni Taasisi chini ya Wizara ya Ujenzi inawatangazia wananchi wote kuwa inatarajia kuendesha kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Udongo/Changarawe kwa Mafundi Sanifu, Wanawake na Vijana kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. Mafunzo haya yatafanyika katika Kampasi ya ICoT - Mbeya kama ifuatavyo: -

| | Jina la kozi | Muda wa Mafunzo | Mafunzo Yatafanyika |
|---|---|---|---|
| 1 | Kozi Maalumu ya Mafundi Sanifu, Vikundi vya Wanawake na Vijana katika Ukarabati na Matengenzo ya barabara za changarawe/udongo (Gravel/Earth Roads) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | Wiki Nne (4) 27/05/2024 – 22/06/2024 | Mkoani Mbeya (ICoT - Mbeya) |

**2. MASOMO YATAKAYOFUNDISHWA:**
Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe/Udongo (Gravel/Earth Roads) kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi:

Kozi hii, Washiriki watajifunza mada mbali mbali kuhusu ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi pamoja na mada shirikishi ambazo ni; utaratibu wa kufungua kampuni, utaratibu wa kujaza kitabu cha zabuni, Teknolojia ya Udongo na Zege Ukarabati na Matengenezo ya Barabara na Usimamizi sehemu ya kazi. Kipekee, kozi hii imelenga kuwawezesha Wanawake na Vijana (washiriki) kupata ujuzi wa kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Recurrent Maintenance'.

**3. NJIA ZA UFUNDISHAJI**
Mafunzo yatafanyika katika awamu mbili; Awamu ya kwanza itakuwa nadharia (Darasani) na Awamu ya pili itakuwa ni mafunzo ya vitendo ('Site').

**4. MALENGO YA KOZI**
Masomo katika kozi hizi yamelenga kumpatia mshiriki mbinu mbali mbali kuhusu matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika:

i. Kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Reccurent, Periodic and Emergency maintenance';
ii. Kufanya na kusimamia kazi za ukarabati wa barabara yaani 'road rehabilitation';
iii. Kuendesha na kusimamia miradi ya matengenezo na ukarabati wa barabara za vumbi/changarawe na barabara za lami;
iv. Kwa wajasiriamali, masomo haya yatawawezesha kujiajiri kwa kufungua kampuni za ujenzi wa barabara zinazotumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi yaani "SPECIALIST CIVIL WORKS-LABOUR BASED CONTRACTORING FIRMS" kisha kupata sifa za kisheria za kununua kazi za miradi ya ujenzi au ukarabati wa barabara zinazotolewa na TARURA au TANROADS.

**5. WALENGWA WA MAFUNZO:**
a) Walengwa wa mafunzo haya ni kwa makundi Maalumu ya Wanawake na Vijana ambao wana adhima ya kuwa wajasiriamali.
b) Mafundi Sanifu wa barabara kutoka ZANROADS – Zanzibar.
c) Watu binafsi wenye uzoefu katika kazi za barabara au majengo na wanaohitaji kujiendeleza na kujifunza zaidi kazi za barabara.

**6. LUGHA YA MAFUNZO:**
Lugha itakayo tumika katika Kozi ya ukarabati na matengenezo ya barabara ya changarawe/udongo maalumu ya vikundi vya wanawake na vijana itaendeshwa kwa kutumia mchanganyiko wa lugha ya Kiingereza na Kiswahili.

**7. ADA ZA USHIRIKI**
Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe/Udongo kwa vikundi vya Wanawake na Vijana
i. Ada ya ushiriki pamoja na huduma za chakula na malazi zinazotolewa na Taasisi ni kiasi cha Tsh. 700,000.
Ada ya ushiriki zilipwe kwa kutumia 'Control Number' itakayotolewa kwa mtu atakayehitaji mafunzo kwa kuwasiliana na uongozi mapema kabla ya kozi kuanza. Inashauriwa kuwa ada ilipwe angalau wiki mbili kabla ya kozi kuanza.

**8. NAMNA YA KUTUMA MAOMBI YA KOZI:**
Wale wote watakao hitaji kujiunga na kozi yoyote kati ya hizi zilizotajwa hapo juu wanatakiwa kutuma maombi yao kwa kutumia anuani ya Posta au barua pepe zilizotolewa hapa chini au wanaweza kupiga simu kwa kutumia namba zilizotolewa kwa kupata maelezo zaidi.

**WASILIANA NASI**

**MKUU WA TAASISI**
**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI ICoT,**

S.L.P 963, MOROGORO.
Simu : 023- 2935229/023- 2935226
: 0762 409087/0787059555/0786 384 062
Nukushi : 023-2935227
Barua pepe : mwti@morogoro.net

S.L.P 1957, MBEYA.
Simu : 025 295 7484/5
: 0764775354/0769317404/0765251509
Nukushi : 025 295 7486
Barua pepe : attimbeya@mow.go.tz, attimbeyafrica@gmail.com

# ‘HII SI SEHEMU YETU NAMUNGO’

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya kushuhudia timu yake ikipata sare ya bao 2-2 dhidi ya Simba juzi, mshambuliaji wa Namungo FC, Kelvin Sabato amesema nafasi ambayo timu hiyo ipo kwa sasa kwenye msimamo wa ligi kuu si sehemu yao.

Akizungumza mara baada ya mchezo huo, Sabato alisema kwa sasa wachezaji wamepania kuhakikisha wanatoka kwenye nafasi waliyopo sasa na kupanda juu kwa sababu hawastahili kuwa kwenye nafasi za chini kutokana na ukubwa wa timu yao.

**Baada ya mchezo wa juzi, Namungo wanashika nafasi ya tisa kwenye msimamo wa ligi wakiwa na pointi 27 baada ya kucheza michezo 24.**

“Tumefurahi sana kupata pointi moja mbele ya Simba, hii inaonyesha sasa tumeamka na kupambana kusaka pointi zitakazotutoa kwenye nafasi hii tuliopo sasa na kusogea mbele, Namungo ni timu kubwa yenye ushindani na kwa kweli hatustahili kuwa kwenye nafasi hii,” alisema Sabato.

Aidha, alisema katika michezo minne iliyopita walipoteza michezo miwili na kutoka sare michezo miwili iliyofuata jambo ambalo linaonesha kwa sasa wanapanda juu.

“Wachezaji tumeamka kwa sasa, hatutaki tena kupoteza mchezo, tumejipanga kwa michezo iliyobakia kupambana kuhakikisha tunasogea kwenye nafasi za juu zaidi,” alisema Sabato.

Katika mchezo huo wa jana uliochezwa kwenye uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi, pamoja na Simba kutangulia mara mbili, Namungo walifanikiwa kusawazisha huku bao moja wapo likifungwa na Sabato.

Baada ya mchezo huo wa juzi, Namungo wanatarajia kuumana na Azam FC kesho kwenye mchezo wa robo fainali ya kombe la Shirikisho la CRDB Bank.




Wafanyakazi wa Taasisi ya UTT AMIS, wakicheza muziki katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani yaliofanyika kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



# *Changarawe atangaza kuhamia ngumi za kulipwa*

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA wa muda mrefu wa ngumi za ridhaa hapa nchini, Yusuph Changarawe ametangaza rasmi kuachana na nmgumi hizo na kuhamia kwenye ngumi za kulipwa.

Akizungumza na Nipashe jana jijini Dar es salaam, Changarawe alisema ameamua kuchukua uamuzi huo baada ya kuona ametunmia muda mrefu kwenye ngumi za ridhaa na umri wake unazidi kusogea.

“Nataka nikirudi kwenye mashindano ya Olympiki mwezi Julai mwaka huu yatakayofanyika Ufaransa nitangaze kustaafu ngumi hizi na kuhamia kwenye ngumi za kulipwa kwani umri umeenda,” alisema Changarawe.

Aidha, aliwapa tahadhari mabondia wa ngumi za kulipwa kutakana na ujio wake kwenye ngumi hizo kutokana na namna alivyojipanga kuuwasha moto kutokana na ubora na uzoefu alionao.

Katika hatua nyingine ameiomba Serikali iwatupie macho wanapokuwa wanakwenda kushiriki mashindano ya Kimataifa nje ya nchi na kuwapa motisha ili wafanye vizuri.

“Ninaomba Serikali itutupie macho tunapokuwa tunasafiri nje ya nchi kushiriki mashindano mbali mbali ya Kimataifa mara nyingi tumekuwa tukishiriki tukiwa kwenye mazingira magumu tofauti na mabondia wengine kutoka Mataifa mengine,” alisema bondia huyo.

# Tembo Warriors waahidi makubwa Misri

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa timu ya taifa ya mpira wa miguu kwa watu wenye Ulemavu Tanzania, ‘Tembo Warriors’, Salvatory Edward amesema ana imani kubwa na timu yake itafanya vizuri kwenye mashindano ya Afrika (AAFCON).

Mashindano hayo yanayotarajiwa kuanza Mei 18, 2024, nchini Misri. Tanzania ipo Kundi D, ikiwa na timu za Angola, Rwanda na Sierra Leone.

Kundi A zipo timu za Cameroon, Misri, Burundi na Nigeria huku Kundi B kukiwa na timu za Liberia, Morocco, Uganda na Senegal na Kundi C kuna timu za Ghana, Kenya, Gambia na Algeria.

Akizungumza na Nipashe jana, kocha huyo alisema ameziona timu zilizopo kwenye kundi lao na kukiri kuwa ni gumu lakini anakiandaa kikois chake kwenda kufanya vizuri.

Alisema kwa kipindi walichokaa kambini wamefanya maandalizi mazuri na bado wanaendelea kufanya hivyo ili kujiweka katika nafasi ya kufanya vizuri kwenye mashindano haya makubwa Afrika.

“Wachezaji wako fiti na naandalizi tuliyoyafanya ninaimani kubwa ya kufanya vizuri katika mashindano haya, tumepata muda wa kutosha wa kucheza mechi za kirafiki na timu mbalimbali za ndani, ili ni jambo zuri kwenye maandalizi yetu” alisema Salvatory.

Aliongeza kuwa anatambua ushindani wa mashindano hayo na wamejipanga kwenda kushindana na kuhakikisha wanafikia malengo yao ya kucheza fainali.

Kikosi cha Tembo Warriors kinatarajia kuondoka nchini Mei 16, mwaka huu kuelekea Misri katika mashindano hayo ambapo mwaka 2022 walifuzu kucheza kombe la Dunian na kuishia hatua ya robo fainali.



Baadhi ya wachezaji wa Tembo Worious mazoezini

## ZISIKUPITE

### SALAH KUBAKI LIVERPOOL

LIVERPOOL ianatarajia Mohamed Salah atasalia katika klabu hiyo na wanataka mshambuliaji huyo wa timu ya taifa ya Misri mwenye umri wa miaka 31 kuwa sehemu ya kikosi chao msimu ujao. ***(The Athletic)***

### KUANDALIWA MKATABA MPYA

MKURUGENZI ajae wa michezo wa Liverpool, Richard Hughes ataongoza mazungumzo kuhusu mkataba mpya wa Mohamed Salah, ambaye mkataba wake wa sasa utaendelea hadi 2025. ***(Times)***

### RASHFORD KWENYE MTIHANI

MARCUS Rashford atakabiliwa na mtihani wa kuamua klabu atakayohamia iwapo ataamua kuondoka Manchester United, huku Paris St-Germain wakisitisha nia yao ya kumnunua mshambuliaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 26. ***(Mail)***

### GUEHI AWINDWA L'POOL

MLINZI wa Crystal Palace mwenye thamani ya pauni milioni 55, Marc Guehi mwenye umri wa miaka 23 ananyatiwa na Liverpool huku klabu hiyo ikimtafuta mbadala wa mlinzi wa Cameroon, Joel Matip mwenye miaka 32, ambaye anatazamiwa kuondoka mkataba wake utakapokamilika msimu wa joto. ***(Football Insider)***

### AJAX YAMTAKA HAG

KLABU ya Ajax ina ya kumteua tena Erik ten Hag kama kocha wao iwapo ataondoka Manchester United msimu huu wa joto. ***(Mail)***

### LOPETEGUI BASI TENA

NIA ya West Ham kumnunua kocha wa zamani wa Hispania, Julen Lopetegui imesitishwa baada ya kujua kwamba AC Milan inataka kumteua kama mbadala wa Stefano Pioli. ***(Guardian)***

### O'HARE ATAKIWA WEST HAM

KLABU ya West Ham inataka kuwasajili winga wa Coventry, Callum O'Hare, 25 na mlinzi wa Hull City, Jacob Graves msimu huu wa joto. ***(Guardian)***

### LEICESTER KUSAJILI

KLABU ya Leicester City inaweza kuwasajili wachezaji wakati dirisha la usajili la majira ya joto litakapofunguliwa licha ya kuwekewa vikwazo na bodi ya Ligi Kuu England. ***(Mail)***

### MAN NA ASHWORTH

KLABU ya Manchester United bado wanapanga kumteua Dan Ashworth kama mkurugenzi wa michezo msimu huu huku wakitarajia kwamba makubaliano ya kulipwa fidia na Newcastle United yatakubaliwa hivi karibuni. ***(Football Insider)***

### DEFOE UKOCHA SUNDERLAND

MSHAMBULIAJI wa zamani wa England, Jermain Defoe, 41, huenda akapata nafasi yake ya kwanza ya ukocha baada ya kufanya mazungumzo na klabu ya Sunderland. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# TEN HAG ATAKA MUDA ZAIDI MAN UNITED

**MANCHESTER,** England

●●● Ni baada ya kuona kikosi chake kikikosa nafasi ya kumaliza 'Top 4' kutokana na...

ERIK ten Hag ameomba 'uvumilivu' baada ya kuthibitishwa kuwa Manchester United wamekosa nafasi ya kuingia kwenye nafasi nne za juu za Ligi Kuu England.

**Hiyo imetokana na sare ya bao 1-1 dhidi ya Burnley Jumamosi (Aprili 27), pamoja na sare ya 2-2 ya Aston Villa na Chelsea, inamaanisha kuwa timu ya Ten Hag haiwezi kumaliza katika nafasi ya tano.**

Akizungumza baada ya kutoka sare na Burnley, Ten Hag, ambaye alijiunga na kikosi hicho akitokea Ajax mwaka 2022, aliwaomba mashabiki na wamiliki wa klabu hiyo muda zaidi wa kurekebisha mambo.

"Tuna wachezaji wachanga sana na hiyo inachukua muda," alisema Ten Hag.

"Tuliijenga kwa kuleta wachezaji wachanga kama Alejandro Garnacho, Rasmus Hojlund na Kobbie Mainoo na wote wako katika msimu wa kwanza wa Ligi Kuu. Ligi inazidi kuwa kali mwaka baada ya mwaka.

"Wachezaji hao wanapaswa kuzoea na hiyo inachukua muda, hivyo tunahitaji uvumilivu."

Ten Hag pia aliashiria mambo ya nyuma ya United kama uthibitisho kwamba subira inaweza kuleta matunda.

Alisema, Sir Alex Ferguson alimaliza msimu wa tatu 2004-05 akiwa na timu iliyojengwa karibu na vijana Wayne Rooney na Cristiano Ronaldo, lakini kufikia 2008 walikuwa wametawazwa mabingwa wa Ligi Kuu mara mbili na kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kutokana na kutoka sare na Burnley, Ten Hag pia alilazimika kushughulikia majibu ya mashabiki kwa uamuzi wake wa kuchukua nafasi ya Mainoo.

Kijana huyo alibadilishwa katika dakika ya 65 na kusababisha mashabiki kadhaa ndani ya Old Trafford kuzomea.

"Ni mashabiki lakini lazima nisimamie timu," Ten Hag alisema.

"Unaona nini mchezo unahitaji na kwa wakati huo na pia ni busara ya kuleta mchezaji ambaye anaweza kushika mpira na ni mbunifu.

"Kobbie, mchezaji mchanga sana, na ulikuwa uamuzi sahihi na unaweza kuona faida ya kuleta miguu mipya ya Scott MCTominay.

"Ninaelewa kuwa mashabiki wanataka kuona ujuzi unaoletwa na wachezaji hao na kuchangia katika timu, ninaelewa hilo, lakini lazima nifanye kazi yangu na huo ni uamuzi sahihi."

# MAN UNITED HAITARAJII OFA KWA RASHFORD




**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imesema haitarajii ofa kwa nyota wake Marcus Rashford, chanzo kiliiambia ESPN kwamba mshambuliaji huyo wa Uingereza hauzwi msimu huu wa joto.

Msimamo wa kifedha wa United unamaanisha kwamba wangezingatia ofa ya pauni milioni 70 kwa Rashford ikiwa zitapokelewa, lakini hawatarajii timu yoyote kufikia bei hiyo. Klabu haitazamii kumtoa mchezaji huyo, chanzo kiliiambia ESPN.

Chanzo kingine kiliiambia ESPN kuna hisia huko Old Trafford kwamba ni PSG pekee ndio wanaweza kukidhi mahitaji ya ada ya United na kufikia ombi la mshahara la Rashford.

PSG wameonesha nia ya kutaka kumsajili Rashford siku za nyuma lakini United wamefahamishwa kuwa hayumo kwenye orodha ya vipaumbele vyao kuchukua nafasi ya Kylian Mbappé msimu huu wa joto. Mbappé anatarajiwa kujiunga na Real Madrid mwishoni mwa msimu huu.

Rashford amekuwa na wakati mgumu msimu huu, akifunga mabao nane pekee katika mashindano yote.

Kuondoka kwa Rashford kungeongeza fedha kwa United kwa sababu mshambuliaji huyo ni mhitimu wa akademi yao, ada hiyo ingewakilisha faida kamili kwenye vitabu na kusaidia klabu kubaki ndani ya kanuni za faida na uendelevu (PSR).

Mhitimu mwingine wa akademi, Mason Greenwood, anatarajiwa kuondoka msimu huu wa joto huku klabu hiyo ikitafuta kumuuza jumla mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22.

Greenwood amefunga mabao 10 akiwa kwa mkopo katika klabu ya Getafe msimu huu lakini kuna uwezekano timu hiyo ya Uhispania itaweza kumsajili jumla.

Chanzo kimoja kiliiambia ESPN kwamba, kama ilivyo kwa Rashford, United haitakubali ada iliyopunguzwa sana na ikiwa matakwa ya klabu hayatatekelezwa, Greenwood anaweza kurudi Old Trafford.



## Guardiola: Michezo mitatu itatupa ubingwa

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Mabingwa wa Soka nchini England, Manchester City, Pep Guardiola amesisitiza michezo mitatu ijayo ndiyo itakayoamua mbio za ubingwa msimu huu.

City wamebakia katika nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi hiyo wakiwa alama moja nyuma vinara Arsenal lakini wakiwa na mchezo mmoja mkononi dhidi ya wapinzani wao hao, huku ikibakiza michezo minne msimu kumalizika.

"Najua michezo mitatu ijayo ni muhimu sana alisema Guardiola akizungumza na BT Sport.

"Ukweli , tuko nyuma ya Arsenal, wako pointi moja mbele yetu." Guardiola aliendelea kusema.

"Sisi ni washindi mfululizo wa ligi, ukipoteza mchezo unasema una muda lakini Arsenal haikuwa hivyo. Wachezaji wanajua ni karibu na kama tunapoteza, hatuna nafasi."

## Tuchel: Tutaitoa Real Madrid kwao

**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA wa Bayern Munich, Thomas Tuchel amesema ni "muhimu tunaamini" baada ya kutoka sare ya 2-2 na Real Madrid kwenye mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya katika Uwanja wa Allianz Arena.

Miamba hao wa Hispania watarejea Madrid kwa mechi ya mkondo wa pili huku wakipewa nafasi kubwa ya kufuzu fainali, lakini Tuchel amesisitiza kuwa sare hiyo itasalia wazi kabla ya mchezo huo wiki ijayo.

"Ni muhimu tuamini," alisema Tuchel.

"Bila shaka inawezekana kushinda Madrid. Bado ni mechi ya 50-50 na nadhani tutaweza kupata nafasi kubwa huko. Lengo liko wazi kabisa, tunahitaji kushinda.

"Tunahitaji kuwa jasiri na kamili ya kujiamini katika mchezo wetu."

Naye kocha wa Madrid, Carlo Ancelotti alidai timu yake haikuwa katika kiwango bora licha ya kumtazama Vinícius Júnior akifunga mabao mawili muhimu kila kipindi. Bayern walitangulia mbele kwa mabao 2-1 kwa mabao ya haraka baada ya muda wa mapumziko, lakini Tuchel alikasirishwa na kile alichoamini kuwa ni nafasi nyingi alizopoteza za kufunga mabao zaidi.

"Matokeo ndio yale, haina mantiki yoyote kujadili kutumia muda mwingi kuhusu hilo," alisema.

"Real Madrid wamefanya hivyo hapo awali, walifunga mabao mawili kati ya nafasi mbili. Sisi sio timu ya kwanza ambayo hutokea, Real Madrid wanafanya hivyo kwa timu kwa hivyo hatupaswi kukata tamaa.

"Tungeweza kufunga la tatu lakini hatukuwa na kiwango cha kutosha. Tulikuwa na nafasi za kutosha za kufunga la tatu na tulifanya makosa kadhaa."

Tuchel pia alirudia utabiri wake wa kabla ya mechi kwamba Serge Gnabry atafunga dhidi ya Real Madrid.



HABARI MICHEZO

## Yanga yawakomalia nyota wake

INATOKA UKURASA 24

kwa udi na uvumba mchezaji huyo kwa ajili ya msimu ujao.

Imeelezwa kuwa baada ya Simba kuhitaji huduma ya beki huyo na kupeleka ofa yao Singida Fountain Gate FC uongozi wa Yanga uligoma kumuachia na kuamua kupandisha dau na kufanikiwa kumpata na kumsainisha mkataba huo miaka mitatu kusalia ndani ya kikosi cha Yanga.

"Ni kweli Kibabage amesaini mkataba wa miaka mitatu na sasa anaendelea kusalia ndani ya Yanga baada ya kuwepo kwa mkopo wa mwaka mmoja akitokea Singida Fountain Gate FC," alisema mmoja wa viongozi wa Yanga.

Baada ya kukamilisha dili hilo tayari wameanza mazungumzo na wachezaji wengine wanaomaliza mikataba yao akiwamo Shomari ambaye anawindwa na klabu ya Azam FC.

Hivi karibuni Rais wa Yanga, Hersi Said alinukuliwa akisema watahakikisha wanamalizana wachezaji wote wanaotaka waendelee kuitumikia klabu hiyo kwa kuwaongezea mikataba.

"Kama tunataka kufanya vizuri ni lazima tuendelee kuwa na wachezaji wetu wenye uwezo mkubwa na kuwaongezea baadhi ili kuendeleza ubora wa kikosi chetu katika Ligi na michuano ya Kimataifa," alinukuliwa Hersi.

Alipoulizwa Ofisa Habari wa Singida Fountain Gate FC, Hassan Massanza, alikiri kuwapo kwa mazungumzo kati ya uongozi wa Yanga na Singida Fountain Gate ya kumnunua jumla mchezaji huyo.

"Ni kweli hilo jambo lipo, tulipokea ofa kutoka klabu mbili ikiwamo Yanga na wao ndio wameonyesha uhitaji zaidi wa kumnunua mchezaji wetu na tayari tumeshafanya nao mazungumzo, kwa sasa tupo kwenye hatua za mwisho kukamilisha sehemu iliyobakia," alisema Massanza.

# MGUNDA: KUNA UPUNGUFU MKUBWA WA KUFANYIA KAZI

**Na Faustine Feliciane**

KAIMU Kocha Mkuu wa klabu ya Simba, Juma Mgunda, amesema yapo mazuri aliyoyaona kwenye kikosi chake lakini kuna upungufu mkubwa unaotakiwa kufanyiwa kazi ili timu kuweza kupata matokeo mazuri kwenye mechi zilizobakia.

Akizungumza baada ya mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Namungo uliochezwa juzi kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruagwa mkoani Lindi, Mgunda alisema ni lazima wafanyie kazi haraka upungufu waliouona ili kuepuka kupoteza pointi.

> **Alisema moja ya mambo aliyoyaona ni kutokuwapo kwa mawasiliano katika safu ya ulinzi ya timu hiyo pamoja na kupoteza nafasi nyingi za kufunga.**

"Hii ndio mechi yangu ya kwanza tangu nimechukua timu, tumecheza vizuri na tuliishika mechi lakini baadhi ya makosa yametugharimu leo",

"Safu yangu ya ulinzi haikuwa na mawasiliano na hii ilipelekea hata kuruhusu goli la kusawazisha kwa wapinzani wetu, tunatengeneza nafasi lakini hatuzitumii, haya yote yanatakiwa kufanyiwa kwazi kwenye uwanja wa mazoezi ili mechi zilizobakia tuweze kufanya vizuri," alisema Mgunda.

Alisema baada ya mchezo huo wa juzi kwa sasa wanajiandaa na mchezo wao wa kesho dhidi ya Mtibwa Sugar.

"Matokeo ya mchezo huu yamepita kwa sasa kama nilivyosema tunarudi uwanja wa mazoezi kujiandaa na mchezo ujao dhidi ya Mtibwa, kama tutafanikiwa kupunguzu mapungufu yetu ni nina uhakika wa kufanya vizuri kwenye mchezo huu," alisema Mgunda.

Kwa matokeo hayo ya juzi, Simba imeendelea kushika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi ikiwa na pointi 47 baada ya kucheza michezo 22 ikizidiwa kwa pointi saba na Azam FC inayoshika nafasi ya pili baada ya kucheza michezo 24 sawa na vinara Yanga wenye pointi 62.



Mshambuliaji wa Simba, Fred Michael (kulia), akiwania mpira na beki wa Namungo FC, Derick Mukombozi, wakati wa mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara juzi kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi. Timu hizo zilifungana mabao 2-2. **PICHA: BINZUBEIRY**

## Simba yaweka rekodi matokeo mabaya

INATOKA UKURASA 24

dhidi ya Namungo FC, Mgunda alikiri kuwapo kwa mapungufu makubwa kwenye timu hiyo.

"Kuna kazi ya kufanya kwenye safu ya ulinzi, tunaruhusu mabao mepesi, mabeki wamekuwa na makosa, hawana mawasiliano na unaweza ukaona hata goli tuliloruhusu na Namungo kusawazisha," alisema Mgunda na kuongeza,

"Inauma, inagusa, lakini siku zote mchezo wa mpira ni mchezo wa kikatili kwa hiyo lazima tukubaliane nayo, pia tumejifunza kitu, tutaenda kukaa chini kutafakari kuona yale yaliyojitokeza, lazima tuweke mambo sawa, safu ya ulinzi lazima iwe imara," alisema Mgunda ambaye ilikuwa ni mechi yake ya kwanza, baada ya kuondoka aliyekuwa Kocha Mkuu, Abdelhak Benchikha raia wa Algeria.

Kwa matokeo hayo, Simba imeendelea kuwa nafasi ya tatu, ikiwa na pointi 47 na kutishia ushiriki wake kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambako wamekuwa wakishiriki mfululizo kwa misimu saba.

Ili kuweza kucheza Ligi ya Mabingwa, Simba italazimika kushinda mechi zake zote zilizobaki, ikiwamo dhidi ya Azam FC, Mei 9.

Kwa msimamo ulivyo na mechi zilizobakia, kama Simba atashinda mechi zake zote zilizobakia (ikiwamo dhidi ya Azam FC), itafikisha pointi 71 na kama Azam itashinda mechi zake zote (ikiwamo dhidi ya Simba) itafikisha pointi 72.

## *KenGold kuzipeleka Simba, Yanga, Uwanja wa Chunya*

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara, timu ya KenGold FC imeazimia kucheza mechi zake kwenye Uwanja wa Chunya uliopo Wilaya ya Chunya Mkoani Mbeya, ambapo Serikali ya Wilaya hiyo na wadau wameahidi kuufanyia maboresho makubwa uwanja huo ili mechi zake zote zikiwemo dhidi ya klabu za Simba na Yanga zichezwe hapo.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mbaraka Batenga, amesema baada ya KenGold kupanda watafanya kila njia ili kuufanyia marekebisho makubwa kwa ajili ya kuuwezesha kukidhi kanuni za Ligi Kuu.

Akizungumza kwenye hafla ya kuipongeza timu hiyo kupanda Ligi Kuu, Batenga alisema halikuwa jambo jepesi kwani walisubiri misimu minne ili kupata fursa hiyo.

"Halikuwa jambo jepesi, tumesubiri misimu minne mpaka kupanda Ligi Kuu na kuchukua ubingwa wa Championship.

"Sasa kinachoendelea ni kwamba tunataka kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara tukiwa Chunya, tunataka kuileta nchi hapa, kwa hiyo wadau wote tushirikiane kwa pamoja, unajua hii ni fursa kwa wakazi wa huku, kuanzia mama lishe, wenye nyumba za kulala wageni, mabasi, bodaboda, bajaji, mahoteli makubwa na huduma nyingi muhimu za kijamii, tushirikiane, tukajipange kwa tukio hili la mara ya kwanza kwenye historia ya wilaya yetu, tunakwenda kuhangaika na ule Uwanja wa Chunya hadi kieleweke, ligi ichezwe huku, Simba na Yanga nazo zije," alisema mkuu huyo wa Wilaya.

Wakati huo huo, uongozi wa klabu ya Tanzania Prisons imeipongeza KenGold kwa kupanda Ligi Kuu kutoka Ligi ya Championship.

Taarifa ya Klabu hiyo imesema kwa kupanda kwa timu hiyo ni fursa nyingine kwa wakazi wa Mbeya kushuhudia burudani kutoka kwa timu hizo mbili za jiji la Mbeya.

"Tunaipongeza KenGold kwa kuwa Bingwa wa Championship, na kupanda Ligi Kuu. Hii ni fursa kwa wakazi wa Mbeya kushuhudia soka safi na burudani kwa timu hizi," ilisema taarifa hiyo ya pongezi.

Michezo
Alhamisi Mei 2 2024
Nipashe



'Tutaitoa Real kwao' UKURASA 22

KAZI KAZI...



Mshambuliaji wa Bayern Munich, Leroy Sane (kushoto), akiwania mpira na kiungo wa Real Madrid, Toni Kroos, katika mchezo wao wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi usiku uwanja wa Allianz Arena mjini Munich, timu hizo zilifungana mabao 2-2. **PICHA: MTANDAO**

# Simba yaweka rekodi matokeo mabaya zaidi

## Yaruhusu mabao mengi zaidi baada ya misimu tisa, wastani wa bao...

**Na Adam Fungamwango**

MABAO mawili iliyoruhusu Simba juzi kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi, imeifanya timu hiyo kuweka rekodi ya kuruhusu mabao mengi kwenye goli lake kwa mara ya kwanza baada ya misimu tisa.

**Katika mechi hiyo ya Ligi Kuu, Simba ilitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Namungo FC na kujiweka kwenye mazingira magumu ya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.**

Timu hiyo imeruhusu mabao 23 mpaka sasa katika mechi 22 iliyocheza, ikiwa ni rekodi mbovu kuwahi kutokea katika mechi zake Ligi Kuu kwa misimu tisa iliyopita.

Mara ya mwisho kuruhusu mabao mengi ilikuwa ni msimu wa 2013/14, ilipomaliza ligi ikiwa imeruhusu mabao 27 katika michezo 26 iliyocheza msimu mzima huku timu 14 zikishiriki ligi katika msimu huo.

Huenda idadi hiyo ya mabao inaweza kufikiwa au kuvunjwa kwani timu hiyo inaendelea kucheza mechi zake za ligi, ikiwa imebakisha mechi nane na takwimu zinaonyesha kuwa bado mabao matano tu ili iweze kuvunja rekodi ya msimu huo ya kuruhusu mabao mengi.

Rekodi zinaonyesha kuwa timu hiyo imekuwa na wastani wa kuruhusu bao moja katika kila mechi mpaka kufikia sasa huku ligi hiyo ikielekea ukingoni sawa na msimu huo wa 2013/ 2014.

Msimu uliofuata baada ya msimu wa 2013/2014, Simba iliruhusu mabao 19 katika michezo 26 iliyocheza huku msimu uliofuata wa 2015/2016 ikiruhusu mabao 17 katika mechi 30.

Wastani wa kuruhusu mabao kwenye lango lake uliendelea kushuka ambapo msimu wa 2017/18 iliruhusu mabao 15 tu katika michezo 30 iliyocheza wakati msimu wa 2018/19 Simba iliruhusu mabao 15 katika michezo 38 iliyochezwa msimu mzima, msimu huo ligi ilishirikisha timu 20.

Msimu wa 2019/20, iliruhusu mabao 21 kwenye wavu, ikicheza mechi 38, 2020/21 na msimu wa 2021/22, iliruhusu mabao 14 uliopita 2022/23, iliruhusu mabao 17.

Takwimu hizo zinaonyesha kikosi hicho ambacho kwa sasa kipo chini ya Kaimu Kocha Mkuu, Juma Mgunda kimekuwa na udhaifu kwenye safu ya ulinzi msimu huu.

Baada ya mchezo wa juzi

INAENDELEA UKURASA 23

# Yanga SC yawakomalia nyota wake

**Faustine Feliciane na Saada Akida**

UONGOZI wa klabu ya Yanga umeanza mchakato wa kuwabakisha wachezaji nyota wake wanaowahitaji ambao mikataba yao inaelekea ukingoni.

Taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo inaeleza kwa kuanzia uongozi wa timu hiyo umemalizana na mabeki wake Nickson Kibabage na Shomari Kibwana ambao mikataba yao ilikuwa inaelekea kumalizika.

Kibabage ambaye yupo Yanga kwa mkopo kutoka klabu ya Singida Fountain Gate, amesaini rasmi mkataba wa moja kwa moja wa miaka mitatu kuitumikia timu hiyo.

Inaelezwa mkataba wa mkopo wa beki huyo unamalizika mwishoni mwa msimu huu lakini kutokana na uwezo aliouonyesha amepewa mkataba huo wa miaka mitatu.

Taarifa za uhakika zilizoifikia Nipashe jana, ni kuwa Kibabage amesaini mkataba huo akitokea Singida Fountain Gate FC na sasa ni mali rasmi ya Yanga na kuzima ndoto za klabu ya Simba ambayo ilionekana kumhitaji



Kibabage

INAENDELEA UKURASA 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042